**TIRA** yaanika masharti ya kulipwa fidia ajali daladala

UKURASA 8



**MFUMO** mpya wa kuzibadili rangi taa za barabarani waja

UKURASA 5



Nipashe

# TESA

Jumanne Julai 11, 2023 TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 12 'Ujane si utegemezi,' aliyefiwa awaambia kinamama wenzake

Ukurasa 13 Ufaulu sayansi, hesabu ni shakani tena kisa, kukosekana mafundi maabara

Ukurasa 14 Ifahamu fedha uitawale, isikuburuze kuishi bila deni ni ushindi kimaisha

TEKNOLOJIA
NA CLAUDIA KAYOMBO, SINGIDA

MBUNIFU MUSA NASORO

## Anayemaliza hofu ya nishati ya kupikia, aja na jiko la mkaa wa kokoto za mawe

KATIKA karne ya 21, moja ya mambo ambayo jamii inayashuhudia ni pamoja na uvumbuzi wa aina mbalimbali maeneo mengi nchini na duniani pia.

Wavumbuzi wanakuja na teknolojia mpya zinazochochea maendeleo ya sasa na siku zijazo, huku nyingine zikihamasisha kulinda mazingira yasiharibiwe.

Mvumbuzi wa jiko sanifu mkoani Singida, Musa Nasoro, ni miongoni mwa wabunifu, anayejitokeza mbele ya jamii kuelezea namna alivyounda jiko linalotumia kokoto au vipande vya matofali ya kuchoma kupikia na kuachana na mkaa na kuni.

Ilikuwa ni wakati wa jukwaa la siku mbili la mashirika yasiyo ya kiserikali (AZISE), mkoani Singida ambalo liliwaleta pamoja wagunduzi na wabunifu, linalofunguliwa na Mkuu wa Mkoa, Peter Serukamba, mapema mwezi huu, akisema mpishi anatumia kokoto za mawe au vipande vya tofali za kuchoma kupika vyakula a aina mbalimbali.

Nasoro anasema pamoja na manufaa mengine jiko hilo ni mwafaka wakati nchi na dunia kwa ujumla inahamasisha jamii kulinda mazingira na kutumia nishati safi na salama.

Anasema matofali hayo huchomwa na mabaki ya mimea kama pumba za mpunga, hivyo hayachomwi kwa kuni.

Anawataka Watanzania kuunga mkono jitihada za serikali kwa kutumia jiko lake kutunza mazingira, lakini kuivisha vyakula kwa muda mfupi. Katika maonyesho hayo alipata fursa ya kumweleza umuhimu wa jamii kutumia jiko hilo sanifu.

"Napenda kuwashawishi Watanzania wenzangu na kwingineko tulinde mazingira kwa kutumia jiko hili ambalo hutumia muda mfupi sana kupikia na bila kuwa na nishati ya gharama. Ukipikia jiko hili ni kwa muda mfupi sana, kwa kutumia vipande vya matofali ya kuchoma au kokoto za mawe na umeme kama ule unaotumia kuchajia simu ambapo utaokoa gharama kubwa za kununua mkaa au gesi," anasema Nassoro.

Akizungumza na Nipashe Nassoro anasema ni miaka mitatu tangu alipovumbua jiko la kwanza huku akibainisha siri iliyochochea uvumbuzi huo kuwa ni changamoto za kimaisha.

Anaongeza: "Nilikuwa napata shida ya kugharamia mkaa pamoja na familia yangu, hivyo nikajiongeza, nikatumia changamoto hii kuwa fursa, nikaanza kutumia ujuzi wangu wa kiufundi kuunda jiko hili."

Akifafanua anasema awali alikuwa fundi redio na saa, kazi aliyokuwa anaifanya kabla ya uvumbuzi huo ya kutengeneza vifaa hivyo ilichangia ufumbuzi wa jiko hilo na kwamba alipata wazo hilo baada ya changamoto ya gharama kubwa za kununua mkaa iliyokuwa anapitia pamoja na familia na jirani zake.

"Nikachukua jiko lile la mkaa, nikaunganisha nyaya mbalimbali na vifaa vingine nikaunda kitu mfano wa injini. Ukitaka kupika unaweka vipande vya matofali ya kuchoma au kokoto za mawe, unatia chenga za mkaa kidogo juu yake, waya kwenye injini unaunganisha na waya ambapo unatumia kuchajia simu ambao ni kiasi cha umeme kama cha kuchajia simu kinatumika wakati wa mapishi hayo."

"Kama huna umeme unaweza kutumia umeme jua (sola), betri ya tochi, ya redio au ya simu kuunganishia hususan kwa eneo lisilo na huduma ya umeme," anasema.

Anaongeza kuwa anakusudia kuimarisha biashara yake katika maeneo mbalimbali ya Tanzania japo anacheleweshwa na uhaba wa mtaji.

Anasema lengo lake ni majiko hayo yawe mazuri na ayauze katika mikoa yote na nje ya nchi akisema moja analiuza kati ya Sh.30,000 hadi 100,000 kutegemeana na ukubwa na kwamba ni imara na anayatengeneza kwa udogo uliochomwa kwa ustadi mkubwa na injini ambayo pamoja na mambo mengine ina feni inayopoza joto kali katika jiko hilo.

MUDA KIDUCHU KUPIKA

Nassoro anabainisha kuwa vipande vya tofali au kokoto zinazopakiwa katika jiko hilo kwa ajili ya kupikia, zinatumika katika kipindi cha wiki tatu na zaidi bila kuweka vingine hali ambayo inaondoa wasiwasi wa gharama kwa mpishi ambaye hana fedha za kununua mkaa au gesi kila wakati.

"Wakati mpishi anapopika kama kuna moto mkali sana anaweza kuunguza chakula, hivyo anazima soketi ukutani kwa vile jiko hutumia kiasi kidogo cha umeme pia ambacho kinaunganishwa kwa kutumia chaji ya simu. Hata hivyo, kila siku nafikiri

INAENDELEA UK.12

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akimsikiliza mbunifu Mussa Nassoro, anayezungumzia jiko sanifu la kokoto za mawe. **PICHA: CLAUDIA KAYOMBO**

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Julai 11, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581368

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## KESI YA KINA MDEE

# 'Kulikuwa na mazingira ya rushwa CHADEMA'



Halima Mdee

UKURASA 3

UKURASA 4



Bwana harusi akiwa na wake zake watatu. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

# Afunga ndoa na wanawake watatu kwa mpigo siku 1



# SERIKALI KUUNGANISHA VIJANA KAMBI ZA JKT KUJITEGEMEA

UKURASA 2

Rais Samia Suluhu Hassan akikagua gwaride maalumu la maadhimisho ya miaka 60 ya kuanzishwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) yaliyofanyika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

**MICHEZO** **YANGA KUJA NA MSHINDO MKUU** UK. 24

**KATUNI** UK. 6




Ujumbe wa Benki ya CRDB ukiongozwa na Balozi wa Tanzania Brussels, Ubelgiji, Jestas Nyamanga, ukipokea Tuzo ya Kimataifa ya Almasi ya Ubora wa 2023 kutoka Jumuiya ya Ulaya ya Utafiti wa Ubora. Sherehe ya kukabidhi tuzo hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki nchini Ubelgiji, Makao Makuu ya Umoja wa Ulaya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuunganisha vijana kambi za JKT kujitegemea

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema serikali itaunganisha Mpango wa Jenga Kesho iliyobora kwa Vijana (BBT) kwenye kambi za mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili kuongeza fursa za kujitegemea na kushiriki shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi.

Akizungumza jana kwenye maadhimisho ya miaka 60 tangu kuanzishwa kwa JKT yaliyofanyika jijini hapa, Rais Samia alisema lengo ni kuwawezesha vijana hao ni watakapohitimu mafunzo kupata fursa ya kushiriki shughuli hizo.

"Lengo la serikali ni kuunganisha shughuli zinazofanywa na JKT kuingia kwenye mpango huu. Tunaposema tunakwenda kukarabati kambi zaidi, kambi tunazokwenda kurekebisha zitaunganishwa katika mpango wa BBT kujengea kesho nzuri ya vijana kinyume cha sasa ambapo vijana wakikosa nafasi ya ajira wanazubaa barabarani."

Alisema mwaka huu idadi ya vijana waliojiunga na JKT imeongezeka na kila mwaka itaendelea kuongezeka.

Pia, alibainisha kuwa JKT inawafunza vijana kuingia katika maeneo mengine ya kazi kwa kujitegemea ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa dira ya maendeleo ya taifa.

"Kwa sasa tunatekeleza dira ya nchi yetu ya mwaka 2020/2025 ambayo imeelekeza kujenga uzalendo, utaifa na umoja, lakini JKT inatekeleza mpango wa tatu wa maendeleo wa miaka mitano unaotekelezwa nchini ambao unatarajiwa kumalizika 2026/2027.

"Mpango huu umeimiza mambo kadhaa lakini jambo kubwa ni kuchagiza kutimiza wajibu wetu wa kutumia rasilimali zetu za ndani ili kuondoa utegemezi bila kusahau mila na desturi zetu. Mpango huo umesisitiza kuendeleza kuimarisha vyuo vya ufundi au stadi za maisha shughuli ambazo nyingi zinafanywa na JKT," alibainisha.

Samia alisema kuwa mpango wa taifa wa miaka mitano unahimiza uwezeshaji vijana ambao umegawanyika katika maeneo mbalimbali ikiwamo kuwawezesha vijana kufunguka kiuchumi.

"JKT imekuwa ikitengeneza ajira jambo ambalo limesisitizwa kwenye mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano, lengo kuwawezesha vijana kupunguza utegemezi ili nchi iweze kujiendesha, serikali inakuja na programu nyingi za kuwawezesha vijana na kwa sasa programu maarufu ni kujenga kesho iliyobora kwa vijana inayowapeleka kwenye masuala ya kilimo, ufugaji na uvuvi," alisema.

Alitoa maagizo kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuandaa mpango mkakati wa kurekebisha kambi zinazohitajika.

Pia, alieleza dhamira ya serikali kuiwezesha SUMA JKT kupata mikopo kwa lengo la kuongeza uzalishaji na endapo kama kukihitajika udhamini, serikali ipo tayari.

Naye Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa, alisema mafunzo ya JKT ni muhimu na yana mchango wa amani iliyopo nchini na wataendelea kushirikiana na wizara za kisekta kuboresha mafunzo ya stadi za kazi kwa vijana wa jeshi hilo ili kupata stadi na maarifa tofauti na ilivyo sasa.

Alisema baada ya mafunzo watakuwa na uwezo wa kujitegemea na kuanzisha shughuli mbalimbali za ujasiriamali, maendeleo ya michezo na sanaa.

"Haya ni maelekezo yako (Rais Samia) kwamba JKT pamoja na jukumu la malezi kwa vijana inapaswa kuwa na ubunifu na kutoa mchango wa uchumi katika taifa letu ili kuzalisha ajira kwa vijana na kulisaidia taifa kuwa na uhakika wa chakula na ili kutekeleza maelekezo yako tunashirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uchumi wa Buluu pamoja na kufungamanisha sekta hizi na sekta ya viwanda," alisema.

Alibainisha kuwa hatua hiyo ni kutekeleza maelekezo ya ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020 ya kuimarisha JKT na JKU ili viwe vyombo vya kuwapatia vijana ujuzi, kujiajiri na kuajiriwa na kuwa vyombo kamili vya huduma ya uzalishaji mali.

Bashungwa alisema JKT imejipanga kuongeza usalama wa chakula nchini na kushukuru serikali kwa kununua mitambo ya kisasa ya kilimo.

Alisema Rais ameongeza bajeti kwa JKT na kuwezesha kuongeza idadi ya kuchukua wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita kujiunga na JKT kwa lazima kutoka 30,000 hadi 52,000.

Awali, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda, alisema Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) limeweka mikakati ya kuliboresha Jeshi la Kujenga Taifa kuwa la kisasa na kwenda na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele, alisema jukumu la jeshi hilo ni malezi ya vijana, uzalishaji mali na ulinzi wa taifa na tangu kuanzishwa kwake Julai 10, mwaka 1963 linatekeleza majukumu kwa ufanisi.

Alisema kwa sasa mafunzo ya vijana yanaendelea kwa operesheni mbili za vijana kwa mujibu wa sheria za operesheni Samia na Venance Mabeyo na operesheni miaka 60 ya JKT kwa vijana wa kujitolea.

Meja Mabele alisema JKT imefanikiwa kubadili fikra za kikoloni kwa vijana waliohudhuria, kujenga umoja, moyo wa kupenda kazi, uadilifu, nidhamu na kudumisha uhuru na amani ya taifa.

Alisema pia JKT imeongeza idadi ya vijana wanaopata mafunzo ya lazima kutoka vijana 11 mpaka 52,000 ambao wapo kambini kwa sasa hatua ambayo imechangiwa na uanzishwaji wa kambi mpya na maboresho ya miundombinu.

Pia alisema katika kuhakikisha JKT inajitegemea kwa chakula na kuchangia usalama wa chakula nchini, inatekeleza mradi wa skimu ya umwagiliaji ambayo iko katika hatua za mwisho za ukamilishaji.

Alisema katika kipindi chote, JKT imejihusisha katika uzalishaji mali kupitia vikosi na Shirika la Uzalishaji Mali (SUMA JKT) katika sekta za ujenzi, kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara hivyo kuchangia gharama za mafunzo ya vijana na kutoa gawio serikalini, kulipa kodi na kuongeza ajira.

## Bilioni 5/- kusomesha waliokatiza masomo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imetoa Sh. bilioni tano mwaka huu wa masomo kwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) kupitia Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP- AEP), kwa ajili ya kusomesha watoto wa kike waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito.

Wakati wa ufungaji wa mafunzo kwa walimu 75 wa sanaa kutoka mikoa 14 yenye vituo vya kufundisha masomo ya sekondari kwa njia mbadala mjini hapa jana, Mratibu wa Mradi wa SEQUIP Kitaifa wa TEWW, Baraka Kionywaki, alisema tayari wanafunzi hao wameshaanza masomo.

Alisema taasisi hiyo imepewa fursa ya kusajili wanafunzi 12,000 hadi mwishoni wa mradi huo wa miaka mitano ambao utekelezaji wake ulianza mwaka 2020.

Alisema kwa miaka miwili ya masomo 2022 na 2023, mradi umeshasajili wasichana 6,949 katika vituo 168 vinavyomilikiwa na taasisi hiyo kusoma masomo ya sekondari kwa njia mbadala.

Kionywaki alisema katika mwaka wa kwanza wa masomo wa 2022 wanafunzi 3,333 walisajiliwa wakati kwa mwaka wa masomo 2023 wanafunzi 3,616 wamesajiliwa.

"Kazi ya kusajili wanafunzi siyo ndogo - hawa takribani 7,000 ndani ya miaka mwili. Niwapongeze walimu na wasichana wenyewe ambao walikatisha masomo na sasa wamerejea kuendelea na masomo yao chini ya mradi huu," alisema Kionywaki.

Alisema wanafunzi 3,616 waliosajiliwa mwaka huu kupitia mradi huo wanatarajiwa kufanya mtihani wa maarifa (QT) Novemba mwaka huu.

Kionywaki alisema wanafunzi wengine 901 kati ya 3,333 waliosajiliwa mwaka wa masomo 2022 wamefaulu mtihani ya maarifa (QT) na kupata sifa ya kufanya mtihani wa kidato cha nne Novemba mwaka huu.

Akizungumzia uboreshaji miundombinu, alisema kila mwaka zinapokewa zaidi ya Sh. bilioni moja kutoka serikalini kwa ajili ya kazi hiyo na mwaka jana (2022) taasisi ilijenga vituo vinne kwa ajili ya wanafunzi wa kike katika mikoa ya Iringa, Rukwa, Pwani na Manyara.

Kionywaki alisema kwa mwaka huu zaidi ya Sh. bilioni moja za kujenga vituo katika mikoa ya Kigoma, Mtwara na Geita zimetolewa, zikiwamo za ukarabati wa majengo na vito vya kufundishia ambavyo kwa sasa vimekuwa vya kisasa.

"Tunamshuku sana Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, ili kuwezesha kusomesha watoto wa kike waliokatisha masomo, ni kazi kubwa ambayo imefanyika na serikali," alisema Kionywaki.

Mwalimu Daudi Mbwambo wa Kituo cha Mkoa wa Kilimanjaro, alimwomba Rais kama alivyoona kuwasaidia hao wasichana, kuwe na mkakati maalum wa kujenga vituo na hosteli maeneo ambayo wanajifunza.

Alisema miundombinu hiyo itakapojengwa itawezesha kuwaweka watoto wao na kupata muda wa kwenda kuwanyonyesha eneo salama kuwalisha chakula, ili wasichana hao wawe na utulivu wakati wanasoma darasani.

Alitumia fursa hiyo kumshukuru Rais kwa kuanzisha mradi huo kwa sababu umewasaidia wasichana wengi nchini ambao wakatisha ndoto zao na kwamba kupitia mradi huo wamejawa na matumaini mapya.

Aliwaomba wadau na watu wengine wenye wasichana waliokatisha msomo na kuwaficha nyumbani, waitumie fursa hiyo kikamilifu kuzifikia tena njozi zao.

Mwalimu Vanson Rongai kutoka Kituo cha Jiji la Mbeya, alisema wasichana hao wanajitahidi kusoma na wengi wamejitambua kutokana na changamoto walizozipata awali.

HABARI KITAIFA

KESI YA KINA MDEE

# ‘Kulikuwa na mazingira ya rushwa Baraza Kuu CHADEMA’

Na Grace Gurisha

MJUMBE wa Bodi ya Wadhamini wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Lucy Mollel (72), ameieleza mahakama kuwa Baraza Kuu la chama hicho lilifikia uamuzi wa kupiga kura ya wazi ya kuwafukuza uanachama Halima Mdee na wenzake 18 kwa sababu kulikuwa na mazingira ya rushwa.

Lucy alidai hayo jana mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wa Mahakama Kuu Masjala Kuu Dar es Salaam wakati anajibu maswali ya dodoso kutoka kwa mawakili watatu wa wabunge hao wa viti maalum, kutokana na kiapo kinzani alichokiwasilisha mahakamani huko.

Mawakili hao ni Ipilinga Panya, Aliko Mwamanenge na Edson Kilatu. Walimwuliza maswali mbalimbali kuhusu Mdee na wenzake kutokupewa nafasi ya kusikilizwa na kisha kufukuzwa uanachama wao.

**WAKILI PANYA:** Katika Katiba yenu ya chama suala la nidhamu kuna kura ya siri na ya wazi?

**LUCY:** Baraza Kuu la CHADEMA liliamua kupigwa kwa kura ya wazi kutokana na mazingira ya rushwa.

**WAKILI PANYA:** Kwa hiyo uamuzi wa kuwafukuza uanachama uliotolewa kutatua tatizo hilo?

**LUCY:** Ndiyo, ulitolewa kutatua tatizo hilo, ndiyo maana kulikuwa na kura ya wazi.

**WAKILI PANYA:** Kwa hiyo kwa sababu hiyo ndiyo baraza likaamua kupitisha kura ya wazi?

**LUCY:** Siyo baraza liliamua tu, ilipigwa kura kwamba kura iwe ya siri au ya wazi kutokana na mazingira na uamuzi huo ulifanikiwa.

**WAKILI PANYA:** Mdee na wenzake 18 wameleta maombi hapa na katika viapo vyao wameeleza kuwa hawakupewa haki ya kusikilizwa na Baraza Kuu na Kamati Kuu.

**LUCY:** Walipewa nafasi na Kamati Kuu ili wajitetee, hawakujitokeza. Wanasema eti wanaogopa usalama wao. Chama kilibadilisha sehemu ya mkutano, lakini bado walikaidi.




Katika Baraza Kuu wakati rufani zao ziliposomwa, waliulizwa mara tatu kama wana chochote cha kusema. Walikaa kimya.

**WAKILI PANYA:** Kwani wewe ni mjumbe wa Kamati Kuu?

**LUCY:** Hapana! Taarifa tulipewa na Mwenyekiti wa Chama, Freeman Mbowe.

**WAKILI PANYA:** Hebu elezea suala la dharura katika katiba ya chama inatakiwa iweje kwa upande wa viongozi.

**LUCY:** Kwenye watu kujichagua wenyewe na kughushi majina na kwenda kuapishwa. Hii imetikisa chama, yaani wanachama wafanye vitu wanavyotaka waachwe, hapana! Lazima hatua zichukuliwe.

**WAKILI PANYA:** Kuna jambo kwamba waliosikiliza rufani yao ndiyo hao hao waliyokaa na kufanya uamuzi wa kuwafukuza uanachama.

**LUCY:** Nusu ya waleta maombi hapa walikuwa wajumbe. Wao nao walishiriki kupitisha katiba. Kwa hiyo, imekuja kuwakamata wao, kwani wao wakati wanaitunga, walikuwa wanamtungia nani?

**WAKILI PANYA:** Ninazo nukuu zako hapa ukiwa mbunge. Ukisisitiza utawala bora wa kufuata kanuni, taratibu na sheria na hapa Mdee na wenzake wanalalamika taratibu zilivunjwa.

**LUCY:** Cheo ni dhamana. Leo unacho kesho huna. Unapokiuka kanuni na taratibu unaadhibiwa bila kufuata cheo chako.

Halafu hao waleta maombi sio wanachama tena wa CHADEMA. Walishafukuzwa hadi sasa sio wanachama tena na mimi sijui kwa nini wako hapa.

**WAKILI PANYA:** Kwani huoni kama kilichofanyika ni kwamba katiba imevunjwa?

**LUCY:** Hawa watoto wameniweka hapa kizimbani na miaka yangu 72 kwa ajili ya wao kukiuka taratibu za chama. Kama wangetii katiba kama mimi, basi leo tusingekuwa hapa.

**WAKILI MWANANENGE:** Waleta maombi wanadai kuwa uliwatumia barua za wito kwa njia ya WhatsApp, kinyume cha katiba ya chama.

**LUCY:** Ni utaratibu ambao unatumika duniani kwa ajili ya mawasiliano ya haraka na pia ipo kwenye katiba yetu kama barua pepe.

**WAKILI MWANANENGE:** Kwenye vielelezo vyenu mlivyoleta hapa mahakamani (video), kwanini hakumleta inayoonesha kwamba mliwapa nafasi ya kuwasikiliza.

**LUCY:** Katika taasisi zote kuna vitu vinavyotakiwa kuwekwa wazi na vingine siri. Ndiyo maana hatujaleta.

**WAKILI KILATU:** Nafasi ya Twaha Mwaipaya katika kiapo chako ni ipi?

**LUCY:** Mimi ninajua tu ushiriki wake katika kumtoa usiku mahabusu Nusurat Hanje na kesho yake kwenda kuapishwa.

Baada ya mawakili hao kumaliza kuuliza maswali, kesi hiyo iliahirishwa hadi Julai 26 mwaka huu saa tatu asubuhi. Jopo hilo litamhoji mjumbe mwingine wa bodi hiyo, Ahmed Rashid Hamis.

Mdee na wenzake walifungua shauri hilo namba 36/2022 Julai 22, 2022, wakiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama na pia iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kusikiliza. Vilevile, Spika na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wasichukue hatua yoyote dhidi yao hadi uamuzi wa mahakama utakapotolewa.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA NA UTATUZI WA MASWALA YA TEKNOLOJIA YA HABARI KATIKA MRADI WA EACOP NCHINI UGANDA NA TANZANIA KUMBUKUMBU NA. REQ-00000292, REQ-00000293, REQ-00000294, REQ-00000295, REQ-00000296

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD (“EACOP LTD”), inaalika kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma na Utatuzi wa maswala ya Teknolojia ya Habari katika nchi za Uganda na Tanzania ili kuwezesha shughuli za kampuni

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili, kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale, katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, Mkoa waTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania na kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda

**MAELEZO YA HUDUMA**

| Kumbukumbu namba ya EOI | Maelezo |
|---|---|
| REQ-00000296 | Miundombinu na usalama wa mtandao pamoja na usimamizi wa matatizo ya mtandao kulingana programu za Cisco, Meraki, FortiGate na SolarWinds |
| REQ-00000295 | Kutoa huduma ya Seva kwa ajili kuhifadhi data yenye uwezo wa kuunganishwa na Microsoft 365 na Azure kulingana program za Dell au inayofanana na hiyo. |
| REQ-00000294 | Urejeshaji wa data kwenye seva kwa kuzingatia programu za Acronis, Veeam au inayofanana na hizo |
| REQ-00000293 | Huduma za ushauri wa usalama wa mtandao |
| REQ-00000292 | Huduma mahususi za usimamiza wa Microsoft 365 na Azure |

Makampuni yanaweza kujibu kwa kuonesha nia katika kumbukumbu namba zote au kuchagua moja kulingana na taaluma au utaalamu
Bidhaa na huduma zinahitajika kutolewa moja kwa moja nchini Uganda na Tanzania. Huduma zinazovuka mipaka ya nchi zinahitajika kutolewa kwa usawa katika chi za Uganda na Tanzania.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Makampuni au taasisi zinazoonesha nia zinaalikwa kutuma maombi kwa kuonenesha eneo au maeneo mahususi ya uhitaji kwa kutaja kumbukumbu namba na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:**

- Cheti cha mtoa huduma kilichoidhinishwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wateja nchini Uganda na Tanzania.
- Marejeleo sahihi ya kutoa huduma katika mradi na huduma sawa na hii
- Apatikane au awe na ofsi katika nchi zote mbili za Uganda and TanzaniaAwe amesajiliwa na awe na leseni stahiki ikijumuisha lakini si tu leseni ya biashara katika nchi za Uganda na Tanzania
- Uthibitisho wa Usajili kwenye Kanzi Data ya Wagavi wa Kitaifa (NSD) nchini Uganda
- Kuzingatia kanuni za Kitaifa za watoa huduma wa ndani za Mkondo wa kati wa mafuta ya Petroli za mwaka 2016 nchini Uganda
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamejisajili kwenye kazi data ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani Tanzania wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia
- Kuzingatia kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa makampuni ya ndani nchini Tanzania
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika katika mkatab.

Makampuni yenye nia, yenye uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya procurement.tz@eacop.com (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya tarehe **27 Julai, 2023 saa 11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) Kichwa cha Barua pepe kiwe **Kumbukumbu na: ( REQ..) – Utoaji wa Huduma na Utatuzi wa maswala ya Teknolojia ya Habari katika mradi wa EACOP nchini Uganda na Tanzania**. Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Makampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

217490802

HABARI KITAIFA

# Afunga ndoa na wanawake watatu siku 1 baada kuachwa

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MKAZI wa Shanwe, Manispaa ya Mpanda, mkoani Katavi, Athumani Yengayenga (35), amewashangaza wakazi wa eneo hilo baada ya kuamua kufunga ndoa na wanawake watatu siku moja.

Amedai lengo lake lilikuwa kufunga ndoa na wanawake wanne kwa siku hiyo lakini mmoja alipata dharura. Amesafiri.

Hali hiyo imeibua maswali na mshangao kwa wakazi wa Mpanda kwa kuwa wengi wao walikuwa hawajashuhudia mtu kuoa wake watatu kwa wakati mmoja, bali wanaoa mmoja na 'kuongeza kidogo kidogo' kwa kadri ya matakwa ya dini kuwa nao wanne.

Bwana harusi huyo aliiambia Nipashe jana kuwa ameamua kufanya hivyo kutokana na maumivu aliyoyapata baada ya kuachwa na mke wake wa kwanza.

Alisema baada ya kuachwa na mke wake huyo, aliona kuna umuhimu wa kuoa wanamke wanne, ili ikitokea ameachwa na mmoja atabakia na wake watatu, ndipo akaanza kuwatafuta wanawake hao kwa nyakati tofauti.

Athumani alisema alifanikiwa kumpata mwanamke wa kwanza Fatuma Raphael na kumwambia anataka kumwoa pasipo kumwambia lengo lake ni kufunga ndoa na wanawake wanne siku moja.

Alisema mwanamke huyo alikubali. Wakawa katika uchumba huku akisubiri ndoa huku akitafuta wengine watatu, ili kukamilisha wanne ambao lengo lake halikutimia baada ya kupata watatu.

Kwa mujibu wa Athumani, hakutaka kusubiri atafute wanne ili ndoa hiyo ifungwe kwa siku moja kwa hofu ya kuwapoteza watatu aliowapata, hivyo aliamua kufunga na waliopatikana huku akiendelea kutafuta mmoja aliyebaki.

Alisema alitumia saa nne kukaa kikao na wanawake hao ili kuwashawishi wakubaliane na wazo lake la kufunga ndoa na wote watatu kwa siku moja. Julai 8 mwaka huu, alifunga ndoa kwenye msikiti mkubwa wa Ijumaa uliopo mjini Mpanda.

Katika familia aliyotoka Athumani, kuoa wake wengi ni kawaida. Baba yake alikuwa na wake 18 ambao aliwaoa kwa nyakati tofauti.

Wakizungumzia ndoa hiyo, wanawake hao walisema wamefurahi kuolewa na wanaona jambo la kawaida, japo mwanzo ilikuwa ngumu kulipokea, hasa kwa mke mkubwa alipoelezwa uamuzi wa mume wake.

"Siku ya kwanza nilipoambiwa mume wangu amepata mwanamke mwingine, niliugua presha ya ghafla, Nikiulizwa ninaumwa nini, sijui ninachoumwa. Nilikuwa na hofu, nilipojua mwanamume kapata mwanamke mwingine nikajua mimi nimeachwa kumbe mwanamume ana lake moyoni na alikaa kimya, hakutaka kuniambia mapema.

"Alivyoongeza mwingine nilitaka ardhi ipasuke niingie inifunike tu. Nikajua kwa huyu mwanamume bahati sina. Nilikuwa nimeanza kujipanga na maisha mengine, alivyosema ninawaoa wote, nilikubali lakini nilikuwa sina matumaini. Je, kuoa wanawake watatu kwa siku moja, lipo kweli au anatuongopea!

"Niliwaambia wazazi wangu na wao walishangaa sana wanawake watatu kwa siku moja. Wakasema 'huyo mwongo, anawadanganya haiwezekani! Na hatujawahi kuona'. Lakini hatimaye siku imefika.

"Kwa kweli nina furaha sana na niliona kawaida sana na hawa ninawachukulia kama wadogo zangu na ndugu zangu, pia na sina kinyongo nao hata kidogo.

"Mimi ninamwomba mume wangu aongeze mke mwingine wa nne. Bado kuna pengo hatujakamilika. Sheria ya dini ni wake wanne. Ninamwahidi mume wangu upendo wa dhati," alisema mke mkubwa, Fatuma Raphael.

"Mimi ni mke wa pili, ninajisikia vizuri baada ya kuambiwa ninaolewa mke wa pili. Niliwaambia wazazi wangu wakanipa ushirikiano na wakanisihi nitoe heshima kwa mume wangu na wazazi wake pia. Nimheshimu na mke mwenza," alisema mke wa pili, Asha Pius.

"Nilipoambiwa ninaolewa mke wa tatu, nilijisikia tu vizuri maisha ni mazuri. Tunapendana tunaheshimiana nimefurahi kupata wake wenzangu wakubwa zaidi ambao hawaringi.

"Mimi niwaambie wanawake wenzangu wasikatae kuolewa uke wenza kwa sababu wanawake ni wengi duniani. Wanaume ni wachache. Wengine wataolewa na nani?" alihoji mke wa tatu, Mariamu John.

Emelida Mwendasila, jirani wa wanandoa hao, alimpongeza kijana huyo na kuomba vijana wengine kuwa na mtazamo kama wake, ili kupunguza mabinti wanaofanya biashara ya kuuza miili yao mtaani.

Alisema ana umri wa miaka 64 lakini hajawahi kuona ndoa ya dini ya Kiislaam mwanamume inafungwa siku moja ya wake watatu kwa mume mmoja.

Mashaka Kakulukulu, Shekh wa Mkoa wa Katavi, alithibitisha kufungisha ndoa hiyo huku akieleza kwamba alifuata taratibu zote za kidini. Dini inaruhusu hadi wanawake wanne.

"Athumani alikuwa ameweka dhamira ya kufunga ndoa na wanne lakini yule mmoja alipata safari ya dharura, hivyo hakuweza kufunga naye ndoa kwa siku hiyo, vinginevyo tungeweza kushuhudia ndoa ya wake wanne kwa mara ya kwanza duniani au Tanzania na Afrika kwa ujumla.

"Athumani kaona aanze na watatu badala ya kuanza na wawili. Kwa hiyo, kwa mujibu wa dini inaruhusiwa. Nilichokifanya katika ufungishaji wa ndoa hii ni kupishanisha muda kama dakika 10 katika kufungisha lakini taratibu zote za dini zilifuatwa," alisema.

Shekh Mashaka alisema jambo hilo ni suna huku akitoa wito kwa jamii na wanawake wa dini ya Kiislam kutowazuia waume zao kuongeza wake pale wanapohitaji.




# CRDB yatunukiwa tuzo ya kimataifa ubora na Taasisi ya Umoja wa Ulaya

**BRUSSELS,** UBELGIJI

BENKI ya CRDB imetunukiwa tuzo ya kimataifa ya ubora na Taasisi ya Umoja wa Ulaya (ESQR).

Tuzo hiyo ilitolewa Jumapili jijini Brussels Ubeligiji, makao makuu ya Umoja wa Ulaya. Hivi karibuni umoja huo ulitoa ufadhili wa Euro milioni 179.35 kwa Serikali ya Tanzania kusaidia mabadiliko ya sera, ukuaji wa viwanda na maendeleo ya miundombinu.

Taasisi ya ESQR inajulikana kutokana na mikakati yake ya kuhamasisha uvumbuzi na ubora katika sekta mbalimbali duniani. Tuzo hiyo ni kielelezo cha jitihada za Benki ya CRDB katika kutoa huduma bora za fedha pamoja na mchango wake mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi pamoja na maendeleo kwa ujumla.

"Tunajisikia faraja na heshima kubwa kupokea tuzo hii kutoka kwa European Society for Quality Research (ESQR)," alisema Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB.

Aliongeza: "Tuzo hii kubwa ni kielelezo tosha cha juhudi na kujitoa kwa wafanyakazi wetu ambao siku zote wana dhamira ya kuhakikisha wanatoa huduma za kipekee kwa wateja wetu.

"Tunapoendelea kutekeleza mkakati wetu wa biashara wa muda wa kati, tumejizatiti kuhakikisha tunaendelea kusimamia ubora na uvumbuzi katika kila tunachokifanya ili tuweze kuwa vinara katika masoko yote tunayoyahudumia."

Alisema kutunukiwa tuzo hiyo ya ubora kwa Benki ya CRDB ni hatua muhimu katika safari ya benki kuhakikisha inakuwa kinara wa ubora katika utoaji wa huduma za fedha.

Alisema tuzo hiyo inaendelea kuiweka Benki ya CRDB katika nafasi bora ya kuwa taasisi ya fedha inayoaminika. Mnamo mwezi Machi 2023, benki ilipokea Euro milioni 150 kutoka kwa Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (European Investment Bank) kwa ajili ya kusaidia biashara changa, ndogo na za kati nchini Tanzania.

Jestas Nyamanga, Balozi wa Tanzania Ubelgiji, alihudhuria hafla ya kukabidhiwa tuzo ya ubora kwa Benki ya CRDB na kuonyesha furaha yake kwa benki ya Tanzania kutunukiwa tuzo kubwa ya kimataifa.

Alisema: "Tunajivunia tuzo hii ya Benki ya CRDB kutoka kwa taasisi hii kubwa ya Ulaya. Tuzo hii inadhihirisha juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuweka mazingira rafiki kwa sekta binafsi ili iweze kufanya vizuri."

Mshauri Mtendaji Mkuu wa ESQR, Michael Harris, aliipongeza Benki ya CRDB kwa kuchukua tuzo hiyo ya ubora kwa mara ya pili baada ya kutunukiwa tena tuzo hiyo mwaka 2021.

"Ninaitakia Benki ya CRDB mafanikio zaidi ili iendelee kuleta utofauti katika masoko inayohudumia lakini zaidi iendelee kuongoza masoko hayo kwa uadilifu, uwazi na kubwa zaidi ubinadamu kwa kugusa maisha ya watu inayowapa huduma," alisema Michael.

Tangu Januari 2023, Benki ya CRDB ilitunukiwa tuzo zaidi ya 13 ikiwamo tuzo ya Benki Bora Tanzania inayotolewa na Global Finance Magazine, Benki Bora Tanzania kwa kuhudumia biashara ndogo na za kati inayotolewa na Global Finance pamoja na Benki Bora ya Kanda inayotolewa na African Banker.

Benki hiyo inaendelea na mikakati yake ya kuchangia ukuaji wa uchumi na kuwezesha watu binafsi na biashara kufanikiwa.

HABARI KITAIFA

# DIT yaja na mfumo mpya taa barabarani

**Na Restuta James**

TAASISI ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) iko katika hatua za mwisho kufunga mfumo wa kisasa wa kuruhusu magari upande wenye uhitaji badala ya utaratibu wa sasa unaomtaka dereva asubiri taa ya kijani imruhusu.

Katika Maonesho ya Sabasaba mkoani Dar es Salaam jana, Mhadhiri Msaidizi wa DIT, Gerutu Bosinge, alisema utafiti wa chuo hicho uko mbioni kukamilisha mfumo huo.

Alisema DIT imekuja na kifaa maalum kitakachotambua upande wenye gari na kuruhusu kwa kuzima taa za kijani za upande usio na magari ili kuuruhusu upande wenye magari uliozuiliwa kwa taa nyekundu.

"Hizi mashine tutazifunga kwenye maeneo maalum na zitafanya kazi zaidi nyakati ambazo hakuna magari mengi kama usiku au alfajiri. Zitabaini upande wenye gari lakini unawaka taa nyekundu kwa kuzima upande ulioruhusu magari kupita," alisema.

Mhadhiri huyo alisema lengo ni kuwasaidia madereva kupita kihalali pale wanapofika katika taa ili kuepusha ajali.

Bosinge aliongeza kuwa chuo hicho kinaendelea na utafiti katika eneo la barabarani ili kuweka mfumo mzuri wa taa utakaowawezesha madereva wa pande zote kutumia vizuri barabara hasa eneo la makutano kwa kuweka taa zinazoruhusu dereva wa kila upande kuingia upande anaoutaka.

"Kama eneo la Fire kuelekea Kariakoo na Muhimbili, mwanzoni wanaotoka Muhimbili walikuwa hawaruhusiwi kukunja kulia, hivi sasa tumeweka mfumo wa taa ambao unawaruhusu," alisema.



# Watatu mbaroni tuhuma za kumbaka mwanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,**
KAHAMA

VIJANA watatu katika Kijiji cha Igumhwa, Kata ya Kitwana, Halmashauri ya Wilaya Kahama, mkoani Shinyanga, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani hapa kwa tuhuma za kuhusika katika tukio la kumbaka mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Kishimba (14).

Inadaiwa kuwa mwanafunzi huyo alitendwa ukatili huo wakati anarejea nyumbani kwao akitokea dukani.

Inadaiwa kuwa vijana hao; wawili ni watoto wenye umri wa miaka 17 (majina tunayo) na Dotto Venancy (18), walihusika kumshambulia msichana huyo mnamo Julai 8, 2023, majira ya saa saba mchana katika kijiji hicho cha Igumhwa.

**Inadaiwa kuwa mwanafunzi huyo alitendwa ukatili huo wakati anarejea nyumbani kwao akitokea dukani.**

Akithibitisha kukamatwa kwa vijana hao Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema jana kuwa baada ya kupokea taarifa hizo, walifuatiliana kuwakamata vijana hao watatu.

Kamanda Mangomi alisema kuwa mmoja wa watuhumiwa hao alitoroka baada ya kutenda unyama huo.

Alisema ukatili huo unatokana na mmomonyoko wa maadili. Mwanafunzi huo anamtambua kwa sura aliyetenda ukatili huo dhidi yake.

Kamanda Magomi alitaka jamii kuwa karibu na watoto kwa kuwalea katika maadili ya kidini, kwa kuwa kumekuwa na kero hizo za mmomonyoko wa maadili katika jamii, hivyo kuwataka kuwa na umakini katika malezi ya watoto.


# NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| TEGETA | ITU COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 93457 KIWANJA NAMBA '1', KITALU 'G' MAPINGA ,KWA JINA LA ANDREW ANTHONY SINDABAHA. 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 89175 KIWANJA NA. '1157', KITALU 'A' TEGETA KWA JINA LA ANDREW ANTHONY SINDABAHA | ANDREW ANTHONY SINDABAHA | 1.MAPINGA BAGAMOYO 2.TEGETA | 18/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | NYUMBA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | UKONGA | 27/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | MARY JOHN DEUS | NYUMBA | MARY JOHN DEUS | KIMARA TEMBONI | 26/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | TRAZIAS BERNARD ISHENGOMA | NYUMBA | TRAZIAS BERNARD ISHENGOMA | MBAGALA MWANAMTOTI | 27/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | DEVOTA JOHN KATINDASA | NYUMBA | MASOUD HAMAD SEIF | KICHANGANI MAJOHE | 27/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | JOHN JAMES MASWI | NYUMBA | JOHN JAMES MASWI | ZAVALA CHANIKA | 27/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ALPHANI JAFARI JUMA | NYUMBA | ALPHANI JAFARI JUMA | MIEMBE SABA -KIBAHA | 09/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | NYUMBA | HASSAN RAMADHANI HARASHI | YOMBO DOVYA-MAKANGARAWE | 10/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | JUMA SHABANI MAGAZI | NYUMBA | JUMA SHABANI MAGAZI | MTAA WA KILIMAHEWA MAILIMOJA WILAYA YA KIBAHA | 09/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | ROGIMWA AGRO COMPANY LIMITED | KIWANJA CHENYE HATI NAMBA 083KYL/1204 | ROGGERS GIDION MWAMENGO NA ANNA DANIEL SANGA | ITETE KYELA MBEYA | 26/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0715868000/0718038313/0753575752/0759282344**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Biashara usafirishaji binadamu ni hatari

**WAKATI** Tanzania ikiwa moja ya nchi duniani zinazopinga biashara haramu ya binadamu, inaelezwa kuwa Mkoa wa Songwe ni mmoja kati ya iliyotajwa kuathirika na biashara hiyo.

Kila mwaka Julai 30, dunia huadhimisha siku ya kupinga biashara hiyo ambayo inaathiri watu wa nchi nyingi huku watoto na wanawake wakiwa waathirika wakubwa.

Watu wanaofanya biashara hiyo hutumia njia nyingi kuwarubuni wazazi wa watoto hao au wanawake wanaowataka kwa kuwadanganya kuwatafutia shule au kazi.

Kwa hapa nchini Mkoa wa Songwe umetajwa kama moja ya mikoa ambayo watu wake wanaathirika na biashara hiyo kwa kusafirishwa kwenda nchi za nje kutumikishwa.

Katibu wa Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Separatus Fella, anafafanua kuwa nchi ina sheria ambayo inazuia usafirishaji haramu wa binadamu na wanaobainika kufanya biashara hiyo huchukuliwa sheria kali.

Mkoa wa Songwe umeonekana kuwa ni sehemu ambayo watu wanasafirishwa kwenda sehemu mbalimbali na wanavushwa mpaka nje ya nchi, wengine wanapelekwa Kenya na nchi zingine kwenda kutumikishwa.

Hata hivyo, serikali inachukua jitihada mbalimbali kwa kuwashirikisha wadau na kutumia mafunzo katika kusaidia kupambana na biashara hiyo pamoja na kufanya mabadiliko ya sheria ambazo zinasaidia katika mapambano hayo.

Katika kuwajengea uwezo wadau mahususi wanaojikita katika kusimamia sheria mbalimbali ikiwamo sheria inayopinga usafirishaji haramu wa binadamu, wadau wakiwamo Jeshi la Polisi, maofisa Uhamiaji, Mahakama, Kazi, Ustawi wa Jamii na wendesha mashtaka, wanapewa mafunzo ya kupambana na biashara hiyo.

Kuna zaidi ya kesi 72 za usafirishaji haramu wa binadamu zimefunguliwa na wahalifu 123 wamehukumiwa huku waathirika 892 waliokolewa.

Mafunzo pia yamefanyika mikoa 19 Tanzania Bara na Visiwani na tayari watekelezaji 2,000 wa sheria hiyo wamepatiwa mafunzo.

"Waathirika wakubwa wa biashara haramu ni wanawake, vijana na watoto ambao hudanganywa kwa kuahidiwa kazi nzuri ikiwamo kuuza maduka mijini katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza na Arusha au nje ya nchi na badala yake hujikuta wakipelekwa kutumikishwa."

Baadhi ya watu wanaorubuniwa na kusafirishwa kwenda nje ya nchi hupata mateso makubwa. Wengine hunyanyaswa kwa kunyimwa chakula, kupigwa na kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Watu wanaowapeleka huko hupata fedha nyingi bila kufuatilia huko walikowapeleka wanaishi vipi.


Wengine wanapofika huko hunyang'anywa pasi zao za kusafiria na wanapopata mateso wanashindwa jinsi ya kurudi nyumbani.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Mbozi, Jeneth Mung'ong'o, anafafanua kuwa usafirishaji haramu wa binadamu una madhara makubwa kwa jamii kwa kuwa watu huenda maeneo ya vijijini na kuwadanganya wanawake na watoto.

Pia uelewa mdogo kwa taasisi zinazohusika na utekelezaji sheria ya kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu ndiyo maana serikali inatumia wadau mbalimbali kufanikisha suala hilo.

Wazazi wanatakiwa kuwa makini na watoto wao wanapofuatwa na watu na kuwarubuni kuwa wanawachukua kwenda kuwasomesha au kuwatafutia kazi mjini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Sera ya Elimu ikabili vikwazo vya wahitimu

**SERIKALI** imeunganisha wadau wa elimu ndani na nje ya nchi, ili kupitia na kutoa maoni ya mwisho katika Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, toleo la 2023 ili kupata andiko linalotarajiwa kutumika rasmi mwakani.

Hatua hiyo imechukuliwa kutokana na kuwapo kwa sintofahamu katika mfumo wa elimu na kusababisha Rais Samia Suluhu Hassan kuelekeza kufanyia kazi, ili kupata sera na mitaala bora itakayowezesha wahitimu kujiajiri na kuisaidia jamii na taifa kwa ujumla.

Ni kweli kwamba, ukosefu wa ajira kwa wahitimu wa vyuo mbalimbali nchini umekuwa ni mjadala wa muda mrefu, kutokana na ukubwa wake, huku likiendelea kuumiza vichwa vya watungaji wa sera na wadau wengine.

Baadhi ya wasomi na wachambuzi walishafikia kuzilaumu taasisi za elimu, kwa maelezo kwamba, zimeshindwa kuandaa wahitimu wao vizuri kulingana na matakwa ya soko la ajira.

Ambacho kimekuwa kikitokea ni ukosefu huo wa ajira au kukosekana, viwanda, kampuni na sehemu za kuajiriwa? Wapo wanaosema kuna kigezo cha uzoefu wa kazi wa miaka mitatu kinachosababisha wengi wao kukosa ajira na kubaki wakirandaranda mitaani.

Ninadhani ujio wa sera mpya ya elimu itakuja mkombozi wa vijana na kuondoa sintofahamu ambayo husababisha wakose ajira au washindwe kujiajiri kutokana na vikwazo hivyo.

Sababu kubwa ya hayo yote, imekuwa ikielezwa na wadau wa elimu kwamba yanatokana na mfumo wa elimu kupitwa na wakati, hivyo kuhitaji kuwapo kwa mabadiliko, ili kuwawezesha vijana kujiajiri au kuajirika.

Ni kweli wanafunzi wamekuwa hauwafundishi kuwa na ujuzi wala stadi zozote za kujitegemea kimaisha, lakini kwa sera inayotarajiwa kutumika kwa ujao, wanafunzi watanufaika na kuwawezesha kutoka hatua moja kwenda nyingine.

Kwa ujumla ni wanafunzi kuhitimu bila ya kuwa na maarifa au ujuzi na stadi za maisha, ni vigumu kuweza kujitegemea na hawawezi kupiga hatua kwenda mbele au kuajiriwa na hata kujiajiri.

Lakini kwa jitihada za jitihada zinazofanywa na serikali na wadau wake, hadi kufikia kuwa rasmi ya sera hiyo ambayo imetolewa maoni na Watanzania kwa ajili ya kuboresha, ninadhani sintofahamu nyingi kwenye elimu zitapungua.

Vilevile uamuzi wa serikali wa kufanya mabadiliko ya mtaala wa elimu vyuoni, unaweza kuleta ufanisi na ujuzi wa ziada kwa walimu ili iwe rahisi kuwasaidia wanafunzi kujitegemea wanapohitimu mafunzo yao.

Lengo kubwa ni kuwafanya wanafunzi kuwa na stadi mbalimbali za maisha, ili kuwanusuru na utegemezi kabla ya kupata ajira, hasa kupitia mtaala ambao umepewa jina la Mafunzo ya Amali.

Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, amewahi kueleza kuwa mafunzo hayo yataongeza ujuzi na vitendo kwa wahitimu, ili waweze kuanza maisha huku taratibu za ajira zikiendelea.

Hiyo inaweza kuwa ni fursa nzuri kwa wanafunzi kunufaika na mtaala ili serikali na wadau wa elimu wanaone matunda kile ambacho wamekuwa wakikikazania ili wanapohitimu waweza kunufaika na elimu walioipata.

Kimsingi, mwanafunzi kuhitimu elimu yake bila ya kuwa na maarifa ya kufanyakazi kwa vitendo, ujuzi au stadi za maisha, ni kikwazo katika maisha ya kujitegemea, kwani ukweli ni kwamba anaweza kukwama kupata ajira au kujiajiri.

Hata hivyo wakati taifa linapozungumzia kukosekana ajira ikumbukwe pia kuwa mabadiliko ya sayansi na teknolojia yameongeza matumizi ya mashine mathalani kompyuta kuchukua nafasi ya binadamu hivyo kupunguza nafasi za kazi.

Kadhalika ukosefu wa vitega uchumi kama viwanda na badala yake bidhaa kuzalishwa nje na kuuzwa kila mahali duniani kupitia soko huria na utandawazi wa kiuchumi nao pia unakwamisha wahitimu na wengine kupata kazi.

Kwa hiyo sera ya elimu iende pamoja na sera ya kuwa na kilimo, viwanda, utoaji huduma, ubunifu na kila aina ya uwekezaji inayozalisha ajira zaidi kuliko ilivyo sasa.

HABARI KITAIFA

## Kikwete ataka watumishi kuwa wabunifu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amesema ili kuwe na maendeleo ni lazima watumishi waachane na utumishi wenye mazoea na kuwa wabunifu kwenye maeneo yao.

Aidha, amesema utumishi mzuri unaweza kuwa chachu ya maendeleo na lazima watumishi wawe wabunifu katika utendaji kazi wao ikiwa ni kutekeleza malengo ya serikali iliyopo madarakani.

Kikwete aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na Watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani pamoja na wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

Alisema lazima kuwe na utendaji ambao utapimwa na kila mtendaji atapimwa kwa uhodari wake wa kufanya kazi kwa kuwa utendaji usio na ubunifu sio ambao serikali inautaka.

"Maelekezo ya Rais anataka watu ambao wanaenda kufanya kazi na wabunifu, kazi zinazofanywa lazima mwisho wa siku kufikia malengo ya wanaohudumiwa," alisema.

Alionya tabia ya baadhi ya watumishi kusemana ovyo kwamba tabia hizo hazipendezi katika utendaji.

Awali, akipokea Taarifa ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Mkoa wa Pwani, alielekeza waratibu wa mfuko huo ngazi ya wilaya nchini kuandaa taarifa zinazoakisi mafanikio na vikwazo vilivyopo.

Alisema taarifa hizo zinapaswa kuwa na uchambuzi wa kina ili kujua mafanikio ya mpango huo na kama kuna vikwazo kwenye miradi iliyotekelezwa ili serikali iweze kufanya maboresho.

Mratibu wa TASAF Mkoa wa Pwani, Roselyne Kimaro, alisema kuwa uhawilishaji wa fedha kwa kaya maskini (CCT) kwa kipindi cha 2023 ni Shilingi bilioni 14.2 zimetolewa kwa walengwa na zimesaidia kuongeza kipato.



Kimaro alisema, mpango wa kunusuru kaya maskini hadi kufikia Juni 2023, kaya zinazonufaika na mpango ni 35,427 kutoka 37,663 na upande wa ajira za muda mpango katika kipindi hicho zimepokewa Shilingi bilioni mbili.

Kwa mujibu wa Kimaro mpango huo umetekelezwa kwa halmashauri nne za Bagamoyo, Chalinze, Kibaha na Kisarawe.



Mwenyekiti wa Shule ya Sekondari ya Bethsaida, Rimond Machari, akizungumza jambo na wanafunzi waliomaliza kidato cha nne kuanzia 2009 hadi 2022 na wengine wanaoendelea kusoma katika shule hiyo iliyoko mkoani Dar es Salaam ambayo inatoa fursa ya elimu kwa watoto wa kike yatima, wanafunzi hao walitembelea shule hiyo jana kwa ajili ya kutoa neno la shukrani baada ya kusaidiwa kutimiza ndoto zao. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# 'Kutozingatiwa matumizi bora ardhi kunasababisha migogoro'

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

WAKULIMA na wafugaji Halmashauri ya Mlimba na Ifakara Mji wilayani Kilombero, Mkoa wa Morogoro wamesema kitendo cha kutozingatiwa kwa matumizi bora ya ardhi kimekuwa kikisababisha kuendelea migogoro ya ardhi kwa makundi hayo.

Waliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara mbele ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Adallah Ulega, uliofanyika Mlimba wilayani Kilombero ambapo walieleza kutozingatiwa kwa matumizi bora ya ardhi ni miongoni mwa sababu zinazochangia migogoro ya ardhi.

Mkulima Jonathan Josephat, alisema kuwa baadhi ya viongozi wa serikali ngazi na vijiji halmashauri hiyo wamekuwa hawazingatii suala la matumizi bora ya ardhi na kuruhusu mifugo mingi kuingia bila utaratibu.

"Baadhi ya viongozi wamekuwa hawatekelezi majukumu yao ipasavyo kwani wamekuwa wakiruhusu mifungo kuingia bila utaratibu maeneo mengi ya vijiji katika halmashauri yetu hii hali inayosababisha kuibuka kwa migogoro baina ya wakulina na wafugaji," alisema Josephat.

Alisema kitendo cha viongozi hao kutozingatia matumizi bora ya ardhi na kuruhusu mifugo kuingia kinyemela kinababisha wakulima wengi kupata hasara kutokana na mazao yao kuliwa na mifugo kila mara.

Mkulima mwingine, Ananias Tomas alisema, viongozi wa vijiji na kata wamekuwa wakiuza ardhi bila utaratibu ili kutoa fursa kwa wafugaji kuingia katika vijiji vyao wakiwa na mifugo mingi ili wapate maeneo ya kulisha.

Alisema kuwa kitendo cha kuuza ardhi kinyemela kinasababisha kuendelea kuwapo migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na wakulima na kwamba viongozi hao wameshindwa kuitatua kutokana na kutanguliza masilahi yao binafsi.

"Kutokana na kutozingatiwa kwa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyetu migogoro ya ardhi imekuwa ikiendelea kuwapo kwani mifugo ni mingi na hakuna malisho ya kutosha hivyo hulazimika kulisha mazao yetu shambani," alisema Tomas.

Mfugaji, Christian Mbanzi, alisema matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyao hayajazingatiwa kutokana na baadhi ya viongozi kutokuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao na aliiomba serikali kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo ili kukomesha migogoro baina yao na wakulima.

Kutokana na changamoto hiyo Waziri wa Mifugo na Uvivu, Abdallah Ulega, alisema serikali inaandaa mkakati maalumu wa kuanzisha ranchi maeneo ya Mkata ili wafugaji wengi waweze kuitumia kupunguza migogoro ya ardhi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alisema serikali haina ugomvi na wafugaji isipokuwa kuingiza mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima kwa makusudi kamwe hawatafumbiwa macho.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# TIRA yakumbusha masharti ya kulipwa fidia inapotokea ajali

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imewataka abiria wanaopanda mabasi au daladala kuhakikisha wanapata tiketi na kukaa kwenye kiti ili ikitokea tatizo, ikiwamo ajali, wapatiwe haki zako.

Ofisa wa Bima wa TIRA Kanda ya Mashariki, Lusungu Mbilinyi, alitoa rai hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari katika Maonesho ya Sabasaba yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam.

Mbilinyi alisema abiria ambaye atapanda katika basi lililojaa au daladala ambamo hatopata kiti, ikitokea ajali hawezi kupatiwa haki zake kwa sababu bima inatolewa kwa kila siti kama inavyooneshwa kwenye kadi ya gari husika na sio kwa watu waliosimama.

"Usikubali kupanda basi bila kuwa na tiketi yenye siti. Hata kwenye daladala ukisimama ina maana ajali ikitokea hautolipwa kwa sababu wamiliki wa mabasi na daladala wanakata bima kwa kuzingatia uwezo wa gari ikiwa ni pamoja na siti zilizopo," alisema Mbilinyi.

Ofisa huyo pia alisema kumekuwa na changamoto ya baadhi ya wananchi ambao wanapata matatizo katika ajali, yakiwamo majeraha bila kupatiwa haki zao. Alisema wataendelea kutoa elimu ili kuwasaidia wananchi wapate haki zao kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa na TIRA.

Mbilinyi alisema kuna malalamiko waliyoyapata kuhusu bima ya mtu wa tatu (third party) ambayo inamlinda mtu ambaye ni mtembea kwa miguu au mwathirika wa ajali ya gari ambaye ni mtu mwingine tofauti na bima na kampuni ya bima.

"Huyu mtu anakuwa hana uelewa wa bima, sheria inataka kila gari linaloingia barabarani liwe na bima. Unakuta watu hawajui utaratibu wa kufuatilia madai yao wanapopata ajali ili wapate stahiki zao," alisema.

Mbilinyi alisema unapokata bima, maana yake unakuwa umepeleka janga husika kwa kampuni, hivyo kampuni ndio inahusika kutoa stahiki za mtu na sio mtu kuingia mfukoni na kutoa fedha zake kwa ajili ya kulipia uharibifu uliojitokeza.

Alisema aliyegongwa, atatakiwa kuwa na hukumu ya mahakama inayoonyesha majina ya waathirika wa ajali pamoja na nyaraka zingine. Hukumu hiyo itawasilishwa kwa kampuni ya bima iliyotoa kinga ya ajali husika ili apatiwe haki zake.

"Uelewa wa mtu aliyepata ajali akiwa na bima hai wengi wao hakuna, mtu akishapata matatizo katika ajali anabaki kimya.

"Sisi kama TIRA tumetoa mwongozo wa viwango elekezi vya fidia ya bima kwa madai ya majeraha ya mwili na vifo kwa mtu wa tatu kutokana na ajali za magari, unaoonyesha mtu aliyegongwa akapata majeraha au kifo anastahili kulipwa kiasi gani," alisema Mbilinyi.

Mbilinyi alisema TIRA ilitoa miongozo minane mwaka jana ikiwa ni pamoja na miongozo inayoonyesha jinsi ya kushughulikia madai kwa kampuni za bima ikitokea mwananchi amepata tatizo kwa wale waliokata bima ya mtu wa tatu.

Alisema mwongozo huo umewekwa kwa lengo la kuweka usawa pamoja na kusaidia walaji na wanufaika wa bima.

"Katika mwongozo huu, TIRA imeweka viwango ikitokea mtu amepata ajali na kufariki dunia aina ya mafao anayotakiwa kulipwa. Ni fedha kwa mtegemezi wake, kugharamikia mazishi na kurudishiwa gharama za matibabu, yaani kama alipelekwa hospitalini na kutibiwa baada ya muda akafariki dunia, gharama hizo zinatakiwa kulipwa," alisema.

Mbilinyi alisema gharama za mazishi kampuni ya bima inatakiwa itoe sio chini ya Sh. milioni moja na wategemezi kupatiwa sio chini ya Sh. milioni 1.5 ikiwa ni maumivu na mateso waliyoyapata baada ya kufariki dunia kwa ndugu yao.

Alisema kazi yao kubwa ni kushughulikia malalamiko ya wananchi endapo hakuridhishwa na huduma ya bima, maana wamezikutanisha kampuni 35 za bima Sabasaba katika 'Kijiji cha Bima'.



Wadau mbalimbali wakichangia damu katika Shule ya St Mary Goreti iliyopo Moshi ikiwa ni sehemu ya shughuli zilizoandaliwa na shule hiyo kuelekea maadhimisho ya jubilee ya miaka 25 ya shule hiyo mwakani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kampuni yaona fursa uwekezaji na biashara

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya CFGT Tanzania inayotoa huduma za usambazaji wa vilainishi vya Kampuni za Puma na Lake Oil nchini, imesema Maonesho ya Sabasaba ni tukio muhimu linaloifungua Tanzania na kuzitangaza fursa kibiashara na uwekezaji.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo katika maonyesho hayo jana aliyataja yana mchango mkubwa katika kuifungua nchi kimataifa.

"Ushikiriki wetu hapa mbali na kuzitangaza huduma na bidhaa zetu kwa washiriki kutoka ndani na nje ya nchi, pia tunaunga mkono kwa dhati juhudi zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kuifungua nchi," alisema Tembo.

Alisema kampuni yake imeridhishwa na uratibu mzima wa maonesho. Washiriki wamekuwa wanatembelea banda lake kutaka kujua huduma mbalimbali zinazotolewa ambayo pia hushughulikia vibali vya kazi na makazi.

"Kampuni yetu ina wataalamu wa kushauri wawekezaji na wafanyabiashara namna wanavyoweza kuwekeza nchini, kuwaongoza kupata vibali vya kazi, ukazi, kuajiri na kupata miongozo ya uwekezaji," alisema Tembo.

Meneja wa Mauzo wa Kampuni hiyo Ilala, Christina Yotham, alisema ushiriki wao utasaidia kutoa elimu na kuhamaisha Watanzania kuchangamkia fursa za kibiashara zilizopo.

"Mwitikio wa washiriki kwenye maonesho ni mkubwa na wengi wao ni vijana ambao ni nguvu kazi ya kesho. Wamekuwa wadadisi wa kutaka kujua namna gani kampuni yetu imeweza kushika soko la ndani na kimataifa," alisema Christina.

## Ushirika nao wajivunia kujitangaza Sabasaba

**Na Elizabeth Zaya**

TUME ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), imesema kushiriki kwake katika Maonesho ya Sabasaba, kunaipa fursa ya kujitangaza, kupata masoko na kujifunza mambo mengi kutoka kwa wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi.

Jana katika maonesho hayo, Mtendaji Mkuu na Mrajis wa vyama hivyo, Dk. Benson Ndiege, alipotembelea katika mabanda ya wana ushirika, alisema:

"Wanapokuja katika maonesho haya kwa bidhaa zao walizonazo, kwanza wanapata masoko, wawekezaji au wafanyabiashara kutoka ndani na nje ya Tanzania. Si hivyo tu, unapokuja hapa pia yapo mengi ambayo unajifunza kwa sababu haya ni maonyesho ya kimataifa na yanashirikisha watu mbalimbali.

"Kwa hiyo, tunapowahamasisha waje hapa tunawaunganisha na masoko, biashara na wanunuzi wa ndani na nje. Lakini nao wanapata fursa ya kutembelea mabanda mbalimbali na wanapofanya hivyo wanajifunza, na wanapata fursa za kuwawezesha kuboresha zaidi yale wanayoyafanya.

"Kama mtu hajawahi kufika katika maonesho haya hawezi kujua anakosa kitu gani, lakini hapa ni mahali sahihi sana kwa ajili ya mwendelezo wa biashara lakini pia kuanzisha biashara."

Alitoa wito kwa wale ambao hawajatembelea katika maonesho hayo, waende kujifunza mambo mbalimbali na fursa zinazopatikana huko.

# Wengi waulizia utaratibu kupima DNA Sabasaba

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) imesema wengi waliojitokeza katika banda lao la Sabasaba wametaka kufahamu huduma zao ikiwamo ya uchunguzi wa vinasaba (DNA) inavyopatikana.

Meneja wa Maabara ya Uchunguzi Sayansi Jinai Baiolojia na Vinasaba wa GCLA, Fidelis Bugoye, alibainisha hayo jana katika Maonesho Sabasaba yanayoendelea Dar es Salaam.

Alisema wananchi hao wanataka kujua huduma ya uchunguzi wa vinasaba. Wanaanzia wapi ili kuipata huduma hiyo na kuelewеshwa.

"Sisi tunawaeleza kwa mujibu wa sheria, kifungu cha 25 kimeeleza ukihitaji kupata uchunguzi wa vinasaba utaanzia ustawi wa jamii au kwa mawakili au kwa mahakama kama jambo hilo lina mgogoro au jambo hilo linahitaji tiba, atawakilishwa na madaktari.

"Wengi wanaofika katika banda letu wana shauku ya kujua huduma zetu na namna ya kuzipata, wapo na wafanyabiashara wanakuja kujifunza na kupata maelezo ya kutaka kufanya biashara ya kemikali. Katika masuala ya uwekezaji kibali anakipataje, ni vitu gani ambavyo anatakiwa kuwa navyo ili aweze kusajiliwa," alisema.

Bugoye alisema huduma ya uchunguzi ya vinasaba kwa mtu mmoja gharama yake ni Sh. 100,000 na majibu yanatoka ndani ya siku 21.

Alisema kuwa katika Kurugenzi ya Sayansi Jinai, wana wajibu wa kufanya uchunguzi na kutumiwa kwenye vyombo vya kutoa haki kama mahakama kwa ajili ya kutoa uamuzi.

"Katika kurugenzi hii, tuna maabara tatu za sayansi jinai na baiolojia ya vinasaba ambayo inafanya kazi ya uchunguzi wa sampuli mbalimbali za kibaiolojia na vinasaba kwa lengo la utambuzi wa binadamu na kuangalia uhalali wa watoto kwa wazazi," alisema.

Bugoye alisema pia wanatoa uchunguzi ambao unasaidia utatuzi wa changamoto za tiba kwa watoto ambao wanazaliwa na jinsia mbili.

"Tunafanya uchunguzi na kutoa taarifa ambayo itasaidia kurahisisha daktari kujua mgonjwa ninayehusika naye ana jinsia ipi yaani ni ya kike au kiume ili aweze kutoa tiba sahihi watoto wanaozaliwa na jinsia mbili," alisema.



## Bonite yapewa kongole kuchangia pato la taifa

**Na MaryMosha,** MOSHI

MBUNGE wa Moshi Mjini (CCM), Priscus Tarimo, ameipa 'kongole' Kampuni ya Bonite Bottlers Ltd ya Moshi (BBL), inayozalisha vinywaji baridi jamii ya Coca Cola, kwa kuchangia pato la taifa, kwa kulipa zaidi ya Sh. bilioni 35 kila mwaka kama majumuisho ya kodi, tozo na makato.

Mwaka jana, kampuni hiyo pia ilipewa tuzo maalum na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kama mlipa kodi bora wa ushuru wa forodha.

Tarimo, aliipongeza Bonite Bottlers mwishoni mwa wiki, alipotembelea na kukagua shughuli za kiwanda hicho kilichoko Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

"Hiki ni moja ya viwanda muhimu sana, kwa mji wetu wa Moshi katika kutoa misaada mbalimbali. Wamekuwa wadhamini wa michezo kama vile mpira wa pete kitaifa, wanaisaidia jamii na kutoa ajira zaidi 1,200 ndani ya kiwanda.

"Nimezungumza nao kwa kina sana, nimeona uzalishaji, ila wanakabiliwa na matatizo ya baadhi ya washindani wao kuzalisha maji ya chumvi na kutumia nembo yao kwa lengo la kuwaharibia soko.

"Hii haijakaa vizuri, nitazungumza na mamlaka ili kutatua hili. Pia wameomba serikali na Bunge, kuja na sheria kali ya usimamizi wa kila kiwanda kulipa kodi kwa wakati ili kuisaidia serikali katika ukusanyaji wa mapato. Nimeyachukua na nitayafanyia kazi."

Msimamizi wa Viwango na Ubora vya Uzalishaji wa BBL, Joel Mbise, aliahidi wanahakikisha uzalishaji unafanyika kwa ubora na viwango vinavyostahili.

Hata hivyo, baadhi ya mawakala wanaofanya biashara hiyo ya vinywaji baridi na Bonite, akiwamo Emmanuel Maleko wa Soko la Kati, Manispaa ya Moshi, alisema kwa sasa uchakachuaji wa maji hayo, umekuwa mkubwa kitu ambacho kinaharibu soko.

# Wakazi vijiji 4 wajiapiza kutolima tena mirungi

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WAKAZI wa vijiji vya Rikweni, Heikondi, Tae na Mahande vilivyoko Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, 'wamejiapiza' ardhi yao haitatumika tena kuzalisha dawa za kulevya aina ya mirungi.

Badala yake wameomba serikali kuwapelekea wataalamu watakaowapa mafunzo juu ya kilimo cha mazao mengine mbadala.

Walitoa ahadi hiyo jana wakati wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe katika vijiji hivyo, baada ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola kuanza operesheni maalum iliyobatizwa jina 'tokomeza mirungi'.

Mkazi wa Kijiji cha Rikweni, Mch. Elisante Senkondo, alisema ardhi yao ina rutuba, hivyo wao kuanzia sasa wako tayari kuachana na kabisa na zao hilo haramu.

"Niiombe serikali itupe nafasi tukae na watu wetu katika makanisa, tuwashauri kwa nguvu zaidi ili kwa hiyari yao wenyewe wakubali kutokomeza hizi dawa za kulevya," alisema.

Aidha, Janeth Sarambo, ambaye ni Mwalimu wa Shule ya Msingi Rikweni, alisema wananchi wengi wa eneo hilo wameathirika kiuchumi kutokana na kilimo hicho kuharibiwa.

"Mwanzo walikuwa hawajagundua ni dawa za kulevya, sasa wamegundua. Tunaiomba serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, ituletee wataalamu wa kilimo, wananchi wapewe elimu kuhusu kilimo cha mazao mbadala kama chakula na biashara.

"Tunaotesha migomba, mahindi, maharagwe ni mazao machache tu hayakubali huku. Tunaomba serikali itusaidie ili wananchi wasipate mahangaiko, walime mazao, wapate biashara na fedha ili wasihangaike na mirungi."

Akiunga mkono kauli hiyo, Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata ya Tae (WEO), Japhet Msengi, alisema: "Tumekuwa tukipambana kwa ajili ya kusaidia jamii inayotuzunguka juu ya athari ya kilimo hiki, ambacho ni cha muda mrefu kwenye kata yetu.

...Tulifanya hivyo kwa muda usiopungua miaka sita tangu tuanze hizi operesheni, baadhi walipunguza na wengine waliendelea kwa madai kwamba kinawanufaisha na kupata pesa.

"Wanadai si kwa ajili ya matumizi bali kuwapatia kipato, tulijaribu ku-organize na taasisi nyingine za kilimo ili kuwasaidia zao mbadala waondokane nacho."

Diwani wa Tae, Samwel Mbwambo, akizungumzia uamuzi huo alisema serikali ina nia njema na wananchi wa kata hiyo, kwa kuwa lengo lake ni kushinikiza wananchi waachane na kilimo hicho chenye madhara makubwa.

"Lakini jamii kupoteza mwelekeo, ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 imeandika utokomezaji wa dawa za kulevya ni sehemu ya wajibu wa serikali.

"Sasa ndugu zangu tuache kabisa, mtafungwa kifungo ambacho ni kikubwa na jamii itapoteza nguvu kazi, vijana wakienda kwenye kifungo itakuwa imeisha."

Pamoja na mambo mengine, Mbwambo, alitoa rai kwa wananchi hao, pia kuhudhuria mikutano ya uelimishaji itakayofanyika ili wapate uelewa utakaowasaidia kubadilika.

Alisema: "Niwaombe serikali, wananchi hawa wametegemea kilimo hiki kwa sababu hawajapata elimu ya kilimo kingine, watusaidia ili tupate mabadiliko makubwa na kizazi kitakachokuwa kizuri."



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Flanone Mining Ltd, Onesmo Mbise, akizungumza na wafanyabiashara wanawake wachekechaji wa madini ya Tanzanite mbele ya Waziri wa Madini, Dotto Biteko, aliyetembelea kitalu C. **PICHA: MARY MARGWE**

# MoCU yaja na uongozi wenye maono, ukuaji chanya

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

CHUO Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), kimeanza 'kuvifunda' vyama vya ushirika na asasi za kijamii nchini, juu ya uongozi wenye maono, ukuaji binafsi katika uongozi, ukuaji chanya katika ujasiriamali na kusimamia mabadiliko katika asasi.

Mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya The Livelihood and Right to Food (LRF), unaolenga kuchangia kupatikana kwa haki ya chakula kwa wanawake, wanaume, vijana na watoto katika nchi za Kenya, Tanzania na Uganda, ifikapo mwaka 2027.

Meneja mradi huo na Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo cha MoCU, Dk. Neema Kumburu, alisema jana kuwa mafunzo hayo yanatekelezwa kupitia mradi wa kuimarisha uwezo wa vyama vya ushirika na mashirika ya kijamii (CACOSMBO), kwa ufadhili wa We Effect East Afrika na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA). "Eneo la pili la mradi huu ni kujenga uwezo wa wanafunzi wa shahada ya awali, zamili na uzamivu kuhusiana na uongozi wa mabadiliko, eneo la tatu ni utafiti wa ufaaji wa uongozi wa mabadiliko kwenye vyama vya ushirika na asasi za kijamii.

Akifungua mafunzo hayo, Makamu Mkuu wa Chuo cha MoCU, Prof. Alfred Sife, alisema nafasi ya MoCU katika utekelezaji wa mradi huo ni kuchangia kuboresha uwezo wa vyama vya ushirika na mashirika ya kijamii, kupita mafunzo ya uongozi wenye kuleta mabadiliko, ufanisi pamoja na utawala wa kidemokrasia.

Alisema: "Programu hii imedhamiria kuleta mageuzi ya ufanisi na kubadilika kwa viongozi na vyama kwa ujumla. MoCU itahakikisha programu ya LFC wanafunzi wa shahada ya uzamili, na wa shahada ya kwanza wanapata kozi zinazohusiana na usimamizi wa vyama vya ushirika na hatimaye MoCU itafanya mapitio ili kubaini kanuni za uongozi na utawala katika harakati za ushirika nchini ili kuboresha utendaji wao kupitia utafiti.


Aliongeza: "Kwenye hili la kuchangia upatikanaji wa haki ya chakula, litafikiwa kwa kuimarishwa kwa mifumo ya chakula na yenye usawa ndani ya jamii.

"Miongoni mwa maeneo ya matokeo ya mradi huu, ni mashirika yenye nguvu, uboreshaji maisha, uimarishaji wa uwezo wa kukabiliana na changamoto, kuimarishwa kwa upatikanaji wa haki, usawa na makazi, kuimarisha usawa wa kijinsia na mfumo wa chakula ulio sawa na endelevu."

Aidha, Meneja wa We-Effect Tanzania, Frank Ademba, akizungumzia mradi huo, alisema katika mwaka 2023/2027, We Effect kupitia programu ya ustawi wa jamii na haki ya chakula, ambayo itafanywa na mashirika 12 Tanzania, inalolengo la kuhakikisha inaongeza ustawi wa jamii kuwa na mifumo endelevu ya chakula.

Alisema: "Huko tutaangalia mifumo halisi ya ustahimilivu wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili mwananchi mwenyewe apate kipato ndani ya kaya.

...Lengo hili limejikita katika maeneo matano ya mpango wa maendeleo wa dunia kwa ujumla, ikiwa ni masuala ya kuondoa umaskini, kuangalia usawa wa kijinsia na ustahilivu na utunzaji wa mazingira."





# Wanahabari wa radio jamii wanolewa maudhui mtandaoni

**Na Alex Sayi,** MWANZA

WAANDISHI wa habari na wahahiri wa radio jamii kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa wamefundwa juu ya kuendana na mabadiliko ya uandaaji wa habari zenye ushindani kwenye mitandao ya kijamii.

Pia wameshauriwa kufuata sheria katika kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Mwanza, Mkufunzi kutoka Shirika la Maendeleo ya Taarifa Nchini (TADIO), Amua Rushita, alisema kuwa kuna haja kwa waandishi wa habari kukuza uwezo wao wa kiuandishi na kupanua wigo wa habari.

Alieleza kuwa lengo la kufanya hivyo ni kuwafikia walaji kupitia habari zilizoandaliwa kwa kuzingatia weledi pamoja na miiko ya taaluma hiyo kupitia mitandao ya kijamii.

"Nyakati zimebadilika tumieni mitandao ya kijamii kuwafikia wananchi kwa kuandaa habari za kuaminika zitakazo watofautisha nyinyi wenye taaluma na wale ambao hawana taaluma ya uandishi," alisema Rushita.

Mhariri wa Lango la Redio kutoka TADIO, Hilali Ruhundwa, alisema kuwa bado tatizo kwa baadhi ya waandishi wa habari kwa redio za jamii kutoona umuhimu wa ushindani uliopo kwa sasa kwenye mitandao ya kijamii.

"Hali hii inasababisha waandishi hao kushindwa kuandaa habari zenye ubunifu, mvuto, ushawishi na ushindani kwenye mitandao hiyo ya kijamii hivyo kufanya vyombo vyao kukosa kuaminika," alisema Ruhundwa.

Naye Ofisa Tathmini na Ufuatiliaji Mafunzo kutoka TADIO, Joan Kanza, alisema kuwa mafunzo hayo yanawasaidia waandishi wa habari wa redio jamii kukuza uwezo wao wa kiuandishi na kuendana na ushindani unaotokana na kukua kwa teknolojia.

Alieleza kuwa shirika hilo litaendelea kutoa mafunzo hayo kwa waandishi na wahariri kutoka redio za kijamii 43 nchini ambazo zinahudumiwa na TADIO lengo likiwa ni kuendana na mabadiliko ya habari mtandaoni. Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo toka mkoani Tabora, Zaituni Juma, alisema kuwa mafunzo hayo yatawasaidia waandishi wa habari kuandaa habari zenye ushindani na kuwa na mawanda mapana ya kuzitumia habari hizo kwa kuwafikia wasikilizaji na wasomaji wengi hata walio nje ya mikoa husika.

Mshiriki kutoka Kahama Shinyanga, Paschal Malulu, alisema kuwa mafunzo hayo yamepanua uelewa wa waandishi ili kuendana na ulimwengu uliko kwa sasa kwa kuwa habari nyingi zimerudi kiganjani na habari moja ikiandaliwa kupitia mitandao hiyo inaweza kusambaa na kuwafikia watu wengi kwa muda mfupi.




Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Mwanza, SF Kamila Labani (kulia), akimvisha cheo cha Koplo wa Zimamoto mmoja wa askari wa jeshi hilo, ZDM/3258 FC Epiana Lutufyo, juzi kwa niaba ya Kamishna Jenerali wa jeshi hilo, John William Masunga, kufuatia kanuni Namba 5 (1) ya Kanuni za Utumishi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji za mwaka 2008 ambapo askari 414 wamepandishwa vyeo nchi nzima. **PICHA: VITUS AUDAX**

## Askari zimamoto wapigwa mawe kisa kuchelewa kufika kwenye tukio

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WANANCHI wa Kata ya Mhongolo Halmashauri ya Mji wa Kahama wamewashambulia askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wilayani humo baada ya kuchelewa kufika katika nyumba iliyokuwa ikiungua ikiwa na watoto wanne ndani.

Kamanda wa Jeshi hilo Wilaya ya Kahama, Mkaguzi wa Zimamoto, Edward Seleman aliiambia Nipashe kuwa walipokea simu ya tukio hilo saa mbili usiku lakini muda huo gari lao lilikuwa kwenye matengenezo, hivyo kuwalazimu kuanza kuomba msaada wa gari la zimamoto kutoka kwenye mgodi wa dhahabu Buzwagi.

Alisema baada ya kupata gari hilo walielekea katika eneo la tukio na ambako baada ya kufika walianza kushambuliwa kwa mawe na wananchi wakidai kuwa wamechelewa kufika katika tukio na kukuta wapo katika hatua za mwisho za kudhibiti moto huo.

"Licha ya shambulio hilo tuliendelea na kazi ya kudhibiti moto huo ili usisambae katika nyumba nyingine za jirani lakini wananchi waliendelea kutushambulia ndipo tukaomba msaada wa askari kutoka kwa Mkuu wa Polisi Wilaya aliyetupatia gari mbili za askari ambao walifanikiwa kuwadhibiti wananchi hao," alisema.

Akizungumzia tukio la moto huo Mwenyekiti wa Mtaa wa Mhongolo, Emmanuel Nangale, alisema kuwa lilitokea majira ya saa mbili usiku ambapo moto ulilipuka juu ya nyumba huku chanzo cha moto huo kikiwa bado hakijajulikani.

Alitaja watoto walionusurika kuwa ni Asha Mohamed miaka (13), Hidaya Pembe (8), Salum Selemani (9) wote wanafunzi wa Shule ya Msingi Mhongolo.

Wengine ni Ilihamu Sulemani mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu, ambaye aliokolewa na mwenzake, Salum Sulemani ambaye alimtoa nje ya geti wakati moto huo ukiwaka.

Mmiliki wa nyumba hiyo, Asha Joakimu ambaye ni bibi wa watoto hao alisema wakati moto huo unatokea alikuwa anatoka kwenye shughuli zake za kila siku.

# Polisi yawaonya wananchi kujichukulia sheria mkononi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limewaonya wananchi wenye tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa kuwaadhibu wahalifu na kusababisha vifo.

Badala yake wametakiwa watoe taarifa katika maeneo husika kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi, Jeneth Magomi, wakati akifunga tamasha la michezo la kupinga vitendo vya uhalifu na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Tamasha hilo lilishirikisha kata 20 za Manispaa ya Kahama lenye kauli mbiu ya 'Kataa uhalifu toa taarifa'.

Alitaja maeneo ambako wanatakiwa kutoa taarifa za uhalifu kwa ajili ya hatua stahiki za kisheria kuwa ni pamoja na ofisi za wenyeviti wa vijiji, kata pamoja na katika kituo cha polisi.

Alisema, kitendo cha kujichukulia sheria mkononi kwa kumshambulia mtu hadi kumsababishia kifo ni uvunjifu wa sheria, hivyo kwa yeyote atakayebainika kufanya hivyo atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufunguliwa mashtaka ya kudhuru mwili hata ya mauaji.

ACP Magomi alisema matukio ya mauaji hususani ya imani za kishirikiana, migogoro ya ardhi, ndoa za utotoni, wivu wa kimapenzi na wizi yanasababisha watu kujichukulia sheria mkononi badala ya kushirikisha serikali za vijiji na mtaa kutafuta ufumbuzi.

Naye Shekhe wa Wilaya ya Kahama, Alhaji Omary Damka, aliwataka wananchi kuacha tabia ya kushirikiana na wezi na kuwaficha watu wasiowatambua na badala yake watoe taarifa ili wawajibishwe.

Diwani wa Ngogwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Kamuri Mayunga, alisema awali wananchi wake walikuwa na tabia ya kujichukulia sheria mkononi wanapokamata mhalifu, lakini tabia hiyo ilikoma baada ya kutoa elimu na kuwaeleza wote wanaohusika na vitendo hivyo kuwa pia ni wahalifu.

Nipashe
# TESA
Jumanne Julai 11, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

## Ifahamu fedha uitawale, isikuburuze kuishi bila deni ni ushindi kimaisha



Ukurasa 12

‘Ujane si utegemezi,’ aliyefiwa awaambia kinamama wenzake



Ukurasa 13

Ufaulu sayansi, hesabu ni shakani tena kisa, kukosekana mafundi maabara

TEKNOLOJIA

NA CLAUDIA KAYOMBO, SINGIDA

MBUNIFU MUSA NASORO

# Anayemaliza hofu ya nishati ya kupikia, aja na jiko la mkaa wa kokoto za mawe

KATIKA karne ya 21, moja ya mambo ambayo jamii inayashuhudia ni pamoja na uvumbuzi wa aina mbalimbali maeneo mengi nchini na duniani pia.

Wavumbuzi wanakuja na teknolojia mpya zinazochochea maendeleo ya sasa na siku zijazo, huku nyingine zikihamasisha kulinda mazingira yasiharibiwe.

Mvumbuzi wa jiko sanifu mkoani Singida, Musa Nasoro, ni miongoni mwa wabunifu, anayejitokeza mbele ya jamii kuelezea namna alivyounda jiko linalotumia kokoto au vipande vya matofali ya kuchoma kupikia na kuachana na mkaa na kuni.

Ilikuwa ni wakati wa jukwaa la siku mbili la mashirika yasiyo ya kiserikali (AZISE), mkoani Singida ambalo liliwaleta pamoja wagunduzi na wabunifu, linalofunguliwa na Mkuu wa Mkoa, Peter Serukamba, mapema mwezi huu, akisema mpishi anatumia kokoto za mawe au vipande vya tofali za kuchoma kupika vyakula a aina mbalimbali.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akimsikiliza mbunifu Mussa Nassoro, anayezungumzia jiko sanifu la kokoto za mawe. **PICHA: CLAUDIA KAYOMBO**

Nasoro anasema pamoja na manufaa mengine jiko hilo ni mwafaka wakati nchi na dunia kwa ujumla inahamasisha jamii kulinda mazingira na kutumia nishati safi na salama.

Anasema matofali hayo huchomwa na mabaki ya mimea kama pumba za mpunga, hivyo hayachomwi kwa kuni.

Anawataka Watanzania kuunga mkono jitihada za serikali kwa kutumia jiko lake kutunza mazingira, lakini kuivisha vyakula kwa muda mfupi. Katika maonyesho hayo alipata fursa ya kumweleza umuhimu wa jamii kutumia jiko hilo sanifu.

“Napenda kuwashawishi Watanzania wenzangu na kwingineko tulinde mazingira kwa kutumia jiko hili ambalo hutumia muda mfupi sana kupikia na bila kuwa na nishati ya gharama. Ukipikia jiko hili ni kwa muda mfupi sana, kwa kutumia vipande vya matofali ya kuchoma au kokoto za mawe na umeme kama ule unaotumia kuchajia simu ambapo utaokoa gharama kubwa za kununua mkaa au gesi,” anasema Nassoro.

Akizungumza na Nipashe Nassoro anasema ni miaka mitatu tangu alipovumbua jiko la kwanza huku akibainisha siri iliyochochea uvumbuzi huo kuwa ni changamoto za kimaisha.

Anaongeza: “Nilikuwa napata shida ya kugharamia mkaa pamoja na familia yangu, hivyo nikajiongeza, nikatumia changamoto hii kuwa fursa, nikaanza kutumia ujuzi wangu wa kiufundi kuunda jiko hili.”

Akifafanua anasema awali alikuwa fundi redio na saa, kazi aliyokuwa anaifanya kabla ya uvumbuzi huo ya kutengeneza vifaa hivyo ilichangia ufumbuzi wa jiko hilo na kwamba alipata wazo hilo baada ya changamoto ya gharama kubwa za kununua mkaa iliyokuwa anapitia pamoja na familia na jirani zake.

“Nikachukua jiko lile la mkaa, nikaunganisha nyaya mbalimbali na vifaa vingine nikaunda kitu mfano wa injini. Ukitaka kupika unaweka vipande vya matofali ya kuchoma au kokoto za mawe, unatia chenga za mkaa kidogo juu yake, waya kwenye injini unaunganisha na waya ambapo unatumia kuchajia simu ambao ni kiasi cha umeme kama cha kuchajia simu kinatumika wakati wa mapishi hayo.”

“Kama huna umeme unaweza kutumia umeme jua (sola), betri ya tochi, ya redio au ya simu kuunganishia hususan kwa eneo lisilo na huduma ya umeme,” anasema.

Anaongeza kuwa anakusudia kuimarisha biashara yake katika maeneo mbalimbali ya Tanzania japo anacheleweshwa na uhaba wa mtaji.

Anasema lengo lake ni majiko hayo yawe mazuri na ayauze katika mikoa yote na nje ya nchi akisema moja analiuza kati ya Sh.30,000 hadi 100,000 kutegemeana na ukubwa na kwamba ni imara na anayatengeneza kwa udogo uliochomwa kwa ustadi mkubwa na injini ambayo pamoja na mambo mengine ina feni inayopoza joto kali katika jiko hilo.

MUDA KIDUCHU KUPIKA

Nassoro anabainisha kuwa vipande vya tofali au kokoto zinazopakiwa katika jiko hilo kwa ajili ya kupikia, zinatumika katika kipindi cha wiki tatu na zaidi bila kuweka vingine hali ambayo inaondoa wasiwasi wa gharama kwa mpishi ambaye hana fedha za kununua mkaa au gesi kila wakati.

“Wakati mpishi anapopika kama kuna moto mkali sana anaweza kuunguza chakula, hivyo anazima soketi ukutani kwa vile jiko hutumia kiasi kidogo cha umeme pia ambacho kinaunganishwa kwa kutumia chaji ya simu. Hata hivyo, kila siku nafikiri

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# ‘Ujane si utegemezi,’ aliyefiwa awaambia kinamama wenzake

## •Alikuwa hohehahe, leo mfanyabiashara kimataifa

KUNA wakati wanawake wanaofiwa na waume huchukuliwa kama waja wasio na mbele wala nyuma, inatokea kwasababu wapo wanaogeuka kuwa omba omba, tegemezi wa misaada na hata kufikia hatua ndugu wa mume na wa upande wao kuwachoka.

Mambo hayo yanajitokeza pale mfiwa anapokuwa tegemezi kwa mume kushindwa kwa hali zote kujishughulisha au kufanya kazi za kujiingizia kipato, kutapatapa na kukwama kimaisha akikwama kupata namna ya kuwalea watoto wake.

Licha ya kwamba wapo baadhi wanaoachwa na mali na kuziuza ili kupata fedha za haraka kumudu mahitaji, lakini nao baadaye hukwama na kugeuka ombaomba kwa vile maamuzi ya kuuza mali pengine hayakufanyika kwa uangalifu na umakini.

Sivyo, kwa mjane Levina Mgalula (49) mkazi wa Bugarama Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, anasema kwake haikuwa hivyo, anaeleza namna alivyokabiliwa na ugumu wa maisha baada ya mumewe kufariki dunia mwaka 2003 na kwamba alikuwa akimtegemea kwa kila kitu bila kuwa na ndoto ya kujishughulisha kuendesha maisha.

Mumewe alikuwa mlinzi wa kampuni hiyo, wakati Levina alikuwa mama wa nyumbani, walikuwa wakiishi nyumba ya kupanga vitu vyote vya kutunza na kuhudumia familia vikifanywa na mumewe bila mama huyo kuhusika moja kwa moja.

Anasema baada ya kuona maisha yake yanaendelea kuwa magumu mwaka 2004 alianza kufanya kazi ya ulinzi katika mgodi wa Barrick Bulyanhulu, ili apate pesa na kuhudumia familia yake.

Anasema mnamo mwaka 2005, wakati akiendelea na kazi yake ya ulinzi alianza kupika chakula na



Mwanamama Levina Mgalula akiwaandalia chakula wafanyakazi wa kampuni zinazofanya kazi na Mgodi wa Barrick Bulyanhulu. **PICHA: MARCO MADUHU**

kuwauzia walinzi wenzake kabla ya kuingia kazini na kujiongezea kipato zaidi.

Anasimulia kuwa wakati akiendelea kutoa huduma hiyo ya chakula kwa walinzi wenzake, wafanyakazi wengine ndani ya mgodi huo kutoka kampuni mbalimbali walipenda mapishi yake na hivyo kuongeza idadi zaidi ya wateja.

Anasema siku ilipotangazwa zabuni na mgodi wa Barrick Bulyanhulu ya kutoa huduma ya chakula kwa kampuni ambazo zinafanya kazi ndani ya machimbo pamoja na polisi, akaiomba kazi hiyo na akaipata ndipo alipoanza kuuaga umaskini.

“Zabuni hii niliipata mwaka 2005 wakati nikiendelea kutoa huduma ya chakula kwa walinzi wenzangu na wanafanya wa kampuni ndani ya mgodi, ndipo nikaacha rasmi kazi yangu ya ulinzi na kujikita zaidi kwenye upishi wa vyaakula mbalimbali,” anasema Levina.



“Mpaka sasa naendelea kutoa huduma ya chakula na maisha yangu ni mazuri tu, naishi kwenye nyumba yangu ninasomesha watoto wangu wawili vyuoni sina maisha ya dhiki tena kama zamani na nimetoa ajira kwa watu wengine ambao nafanyanao kazi za upishi,” anaongeza mama huyo wa watoto wawili.

Anaishukuru Barrick Bulyanhulu kwa kumwamini na kumpa nafasi ya kuendelea kutoa huduma hiyo ya chukula hadi sasa na kubadili mfumo mzima wa maisha yake.

Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 inazielekeza kampuni kutoa kazi kwa wazawa zikiwamo za huduma (Local Content) na ndivyo imekuwa ikifanya Barrick Bulyanhulu kutoa fursa kwa wananchi ambao wanauzunguka mgodi huo na kujikwamua kiuchumi.

Mrakibu kutoka Idara ya Uhusiano kwa Jamii Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, William Chungu, anasema mwanamama huyo alipata zabuni ya kulisha wafanyakazi wa kampuni mbalimbali kama za usafi ofisini na vyooni, za ulinzi zikiwamo za kampuni binafsi, ujenzi, kusafirisha wafanyakazi na kutunza mazingira pamoja polisi kutokana na kuandaa chakula chenye ubora zaidi.

Anasema vyakula wanavyoandaa vinapimwa viwango na maofisa wa afya na kwamba mlo lazima uwe umekamilika ukiwa na aina zote za vyakula mboga pamoja na matunda.

Anasema pia wapo kinamama wengine sita, ambao wamepata kazi ya kutoa huduma ya chakula kwenye matukio mbalimbali ya kijamii ambayo huandaliwa na mgodi huo, ili kuwawezesha na kuwa kwamua kiuchumi na kuendesha familia zao na kuacha kuwa tegemezi kwa waume zao.

Chungu anasema, kwa upande wa wafanyakazi wa mgodi wa Barrick Bulyanhulu, wanahudumiwa chakula na kampuni nyingine ambayo pia ni ya wazawa na huduma hizo nyingi huchukua vifaa na mahitaji kutoka kwa wananchi wanaouzunguka mgodi, vikiwamo vikundi vya kinamama ambavyo vinalima mboga vilivyowezeshwa na mgodi huo.

Anawataka wajane kuamka, kushirikiana na kutafuta njia bora za kuendeleza maisha yao badala ya kuwa wategemezi maana hata unyanyasaji unatokana na wengi kuwa wategemezi na kurudi nyuma.

## ANAYEMALIZA HOFU YA NISHATI YA KUPIKIA, AJA NA JIKO LA MKAA WA KOKOTO ZA MAWE

INATOKA UK.11

namna ya kuboresha jiko hili nataka liwe la viwango vya juu zaidi ya lilivyo sasa,” anasema Nassoro.

Anasema sasa anatengeneza majiko mengine makubwa ambayo yatawawezesha wafanyabiashara wa viazi vya kukaanga au chips, na wa nyama choma kuyatumia na hivyo kuwaepushia gharama ya kutumia mkaa na kuendelea kuharibu mazingira. Kuhusu kuwapa vijana fursa za ajira anasema ndiyo lengo lake hasa kwani anataka awe na kiwanda na kwamba yeye awe msimamizi wa kuwaangalia wafanyakazi vijana atakaowaajiri.

“Nina kijana mmoja ambaye anafanya kazi hii, lengo langu niwafundishe vijana wengi na nijenge kiwanda kikubwa kwa ajili ya kazi hii,” anasema Nassoro na kuongeza kuwa kwa ujumla maisha yake ya sasa yana tofauti kubwa na ya wakati ule alipokuwa akitengeneza saa na redio kwani kipato chake kilikuwa cha chini zaidi. Sasa sitengenezi tena redio na saa, kazi yangu ni haya majiko ambayo yananipa kipato kinachoridhisha na naamini siku zijazo hali yangu kiuchumi itakuwa nzuri zaidi ya ilivyo sasa,” anabainisha.

Aidha, pamoja na ubunifu huo anasema akipata fedha anakusudia kwenda Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), kuongeza ujuzi na ana uhakika ataongeza maarifa zaidi kwa kuwa kuna wataalamu wa aina mbalimbali na washauri japo anasema kinachomchelewesha ni fedha, lakini anafurahia kuvumbua jiko hilo na kwamba anachofanya kutafuta mtaji ambao utaboresha kazi yake na kupanua wigo wa biashara hiyo ndani na nje ya Tanzania.

ELIMU
NA SABATO KASIKA

# Ufaulu sayansi, hesabu ni shakani tena kisa, kukosekana mafundi maabara

## •Walimu wageuka 'lab technicians'



Mwanafunzi Fatuma Ally akitoa malalamiko yake kuhusu ukosefu wa wataalamu wa maabara.

NI wasiwasi wa muda mrefu kuwa wanafunzi wengi hawafanyi vizuri katika masomo ya sayansi pamoja na hisabati hasa katika shule za sekondari za serikali.

Changamoto zinazowaathiri zinatajwa kuwa ni uhaba wa walimu na ukosefu wa maabara na vifaa katika shule za sekondari za umma za mijini na vijijini.

Baada ya upungufu kuibuliwa, hatua zinachukuliwa kwa kuongeza walimu wa sayansi na hesabu na kujenga maabara za kisasa kwenye sekondari hizo kazi ikifanyika zaidi katika awamu ya nne.

Hata hivyo shida ya kukwamisha wanafunzi kujifunza sayansi na hesabu kikamilifu imerudi kwa sura nyingine tofauti nayo nayo ni upungufu wa wataalamu wa maabara (laboratory technicians).

Wataalamu au mafundi wa maabara ndiyo wanaotayarisha vifaa na vitu vinavyotumiwa kufanya majaribio (test), hutengeneza na kuandaa 'solutions' na vimiminika vingine, slaidi, vitabu na vifaa, kusafisha na kutunza maabara na kusaidia walimu kufanikisha kufundisha kemia, fizikia, bailojia na kilimo kwa wanafunzi wa ngazi mbalimbali ni haba.

Uhaba unaibuliwa na mwanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya Sekondari Abuu Juma iliyopo Kivule Dar es Salaam, Fatuma Ally, anayesema hawana wataalamu wa maabara shuleni.

"Shule yetu haina wataalamu wa maabara, badala yake wanatumika walimu ambao kimsingi si wataalamu, sasa katika mazingira hayo hatuwezi kupata mafunzo kiufasaha," anasema Fatuma.

Ni katika kikao cha bunge la wananchi kilichoitishwa na vituo vya taarifa na maarifa vya Kivule na Majohe kwa uratibu wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), kujadili bajeti kuu ya serikali ya mwaka 2023/24 kama imezingatia mrengo wa kijinsia katika sekta mbalimbali.

Mwanafunzi huyo anakuja na hoja hiyo, akisema serikali inajitahidi kujenga majengo na kuweka maabara, lakini ukosefu wa mafundi maabara ni kikwazo cha kujifunza na kufaulu sayansi.

"Ni vigumu walimu wa kawaida kutumia maabara hizo kwani hawana ujuzi, badala yake wanafundisha juu juu. Hatuwezi kufanikisha azma ya kuwa na mafanikio kwenye elimu kwa vitendo bila kuwa na mafundi hawa," anasema Fatuma.

**CHAKULA SHULENI**

Pamoja na kwamba bunge hilo lilikuwa likijadili bajeti hiyo katika sekta mbalimbali, mjadala mkubwa uligeukia changamoto za zilizopo kwenye elimu, huku suala la chakula shuleni, taulo za kike na uhaba wa matundu ya vyoo nao ukachua nafasi kubwa.

Mwalimu Nteghenjwa Mbwambo wa Shule ya Msingi Mji Mpya jijini anasema shule hiyo inakabiliwa na uhaba wa chakula, kwa kuwa baadhi ya wazazi na walezi hawachangii mlo kwa ajili ya watoto wao.

"Chakula shuleni kinaongeza usikivu na utulivu darasani, lakini baadhi ya wazazi hawatoi fedha za chakula, hali ambayo inasababisha maendeleo ya wanafunzi kuwa duni kutokana na njaa," anasema Nteghenjwa.

Anataja changamoto nyingine kuwa ni ukosefu wa taulo za kike ambao husababisha baadhi ya wanafunzi wasihudhurie shule kwa zaidi ya siku tatu kwa kuwa wanakosa namna ya kujisitiri.

"Ombi langu kwa serikali ni kwamba itoe chakula kila shule na pia igawe taulo za kike bure kama inavyogawa mipira ya kiume kondom, kwenye maeneo ya starehe," anasema Mwalimu .

Mwanafunzi wa kidato cha nne Shule ya Sekondari Kerezange, Jacqueline Jairo, anasema shuleni kwao wanafunzi wa kike wanakosa sehemu ya kujihifadhi wakati wa siku za mwezi.

"Pamoja na kuwa na matundu ya vyoo, ni vyema tujengewa chumba maalum cha kujihifadhi kikiwa na taulo, ili tuondokane na tatizo hili la kutohudhuria masomo," anasema Jacqueline.

Mjumbe wa bunge hilo, Joseph Safari, anasema shule nyingi zina uhaba wa matundu ya vyoo, hali inayosababisha kero kwa wanafunzi.

"Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 inaelekeza kuwa tundu moja la choo linatumika wasichana 20 wakati kwa wavulana uwiano ni wanafunzi 25 wa kiume, lakini Shule ya Msingi Majohe ina wanafunzi 3,600 na matundu 17, kwa idadi hiyo haiwezekani," anasema Safari.

**WAZAZI WAWA 'ATM'**

Mzazi Pendo Magesa analia na 'twisheni' akidai kuwa wanafunzi katika shule nyingi za umma wanatozwa fedha kuanzia Shilingi 500 hadi 1,500 kwa ajili ya masomo ya ziada bila ridhaa ya wazazi au walezi.

"Mtoto asipokwenda na fedha anachapwa. Nisaidie kuelewa, hivi serikali imerejesha twisheni? Kama ndivyo, ni sawa kumchapa mtoto asiyekuwa na fedha?" anasema Pendo.

Aliyekuwa spika wa bunge hilo la wananchi Idd Nyange, anasema anayachukua malalamiko yote na atayafikisha serikali ya mtaa nao utayafikisha kata, ili yapelekwe ngazi za juu kufanyiwa kazi.

"Lakini kuibuka suala la 'twisheni' kwamba wazazi na walezi wanatozwa fedha kila siku na wasipotoa, watoto wao wanachapwa, sidhani kama ni vizuri walimu kufanya hivyo," anasema Nyange.

Anafafanua kuwa hajajua kama serikali imeruhusu 'twisheni', na kwamba kwa kawaida kamati au bodi za shule ndizo hufanya maamuzi ya jambo lolote kwa niaba ya wazazi, walezi na wanafunzi.



Wananchi wakifuatilia bunge lao. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Ifahamu fedha uitawale, isikuburuze kuishi bila deni ni ushindi kimaisha

• Uwekezaji bora ni juhudi ufanyazo kupata maendeleo



MAISHA ya mwanadamu kawaida yanaelezwa kuwa yanazungukwa na mambo kama kupata mshahara, kuweka au kuweka akiba, kugharamia mambo mengi ya kila siku kuanzia umeme, maji, makazi, kulipa madeni na kujaribu kuendeleza utajiri kama upo.

Mtaalamu wa masuala ya kifedha Brian Tracy, wa nchini Marekani, anasema kwamba kadiri unavyoelewa kikamilifu pesa ndivyo maisha yako yatakavyokuwa bora, akiandika kitabu kiitwacho 'Sayansi ya Pesa' na kuelezea kwa kina kuhusu fedha za mtu binafsi.

Akianza maisha kama kibarua, Tracy amepanda juu kimafanikio, leo ni mkuu wa kampuni yenye kampuni nyingi zinazoongoza kwa kupata wateja kutoka na kazi zilizokuwa zikifanyika

Amekuwa kinara wa kufunza na hadi sasa wafanyakazi na maofisa wa mashirika takribani 250,000 wamehudhuria semina zinazoendeshwa na msomi na mwandishi huyo kuhusu mada mbalimbali za mambo ya kutawala pesa.

Anawapakulia masuala mbalimbali na kuwaletea mafunzo aliyopata kutokana na matukio mengi aliyoyaona na kujifunza katika safari yake ya maisha katika mfumo wa kitabu kilichoitwa 'Sayansi ya Pesa'.

## KUDHIBITI GHARAMA

Tracy anasema kuwa kuishi bila deni ni nusu ya kushinda vita vya matatizo yanayokukabili maishani mwako na kwamba ukipunguza gharama, hautaingia kwenye deni, akipendekeza njia kadhaa kuu za kufanya hivyo.

Anasema muhimu kati ya hayo ni 'kuahirishwa kufanya manunuzi yasiyo ya lazima kwa siku 30 au mwezi na hiyo inamaanisha kuwa ikiwa ungependa kununua bidhaa yoyote ya kifahari au isiyo ya lazima, unapaswa kuiahirisha kwa siku 30.

Hata baada ya siku hizo au mwezi kupita ikiwa unahisi haja ya bidhaa hiyo, basi ndipo unapaswa kununua, akisema mojawapo ya sababu kuu za kuongezeka kwa matumizi bila udhibiti ni kununua vitu ambavyo havihitajiki tena ukifanya hivyo kwa kukurupuka.

Kwa mujibu wa Tracy, njia hii ya siku 30 ya kuahirisha inaweza kuepusha hatari hiyo ya kuwa na madeni na kununua bidhaa au mali kwa kurupuka bila kuwa na bajeti au mpango wa kufanya hivyo kisa tu kusikiliza kile roho inachotamani.

## UWEKEZAJI BORA

Brian Tracy anasema uwekezaji bora ni wakati na juhudi unazoweka katika maendeleo yako au yetu na kwamba wengi wanahangaikia mapato kutokana na shughuli nyingine zaidi ya kazi.

Aidha, hutumia muda wao mwingi katika shughuli hizo, akisema hilo si wazo zuri au bora, anza na wewe mwenyewe.

Ikiwa wakati huo huo unatumika katika kuboresha ujuzi uliopo au kujifunza maarifa mapya, mapato yataongezeka mara nyingi, kwa mfano, Tracy anaeleza katika kitabu chake kwamba muda ambao wafanyakazi hutumia katika biashara ya ndani unaweza kutumika vyema zaidi katika kazi zinazohusiana na shughuli wanazofanya au kazi zao.

## ACHA MAZOEA

Anasema maisha ya mwanadamu ni mkusanyiko wa mazoea, akiamini kuwa mwanadamu siyo kiumbe wa kijamii tu bali pia mtumwa wa tabia zake.

Anasema kwa mifano mingi kwamba mazoea hutawala maisha ya mtu mfano fikiria juu ya maendeleo kuwa tabia zako. Unapaswa kutenga muda fulani kila siku kwa lengo lako la kesho na kwamba hata

katika safari ya kutafuta fedha binafsi, unaweza kupata uhuru wa kifedha ikiwa tu unakuwa na tabia nzuri na kuifanya kuwa sehemu ya maisha. Tracy anapendekeza kwamba matumizi yanaweza kudhibitiwa kwa kubadilisha mazoea machache.

Anakumbusha kuwa kuna tofauti kati ya mshahara, kipato na mali na kwamba mshahara wetu sio utajiri wetu, akisema unahitajai kuelewa hilo vizuri zaidi.

Anafafanua kuwa wengi wako chini ya dhana potofu kwamba mshahara mkubwa unamaanisha utajiri zaidi, na kwamba ukiongezeka, gharama pia zitaongezeka na kusisitiza kuwa hilo ni jambo la kuzingatia.

Baada ya kufanya uwekezaji mwingine katika mshahara unaopata, kiasi kinachobaki kinapaswa kutumika kwa matumizi mengine.

Anasema na katika suala hilo, Tracy anamtaja Warren Buffett kama aliyeishi katika nyumba moja ndogo kwa miongo kadhaa. Buffett amekuwa mmoja wa watu tajiri zaidi duniani kwa miaka mingi amekuwa akikaa katika nyumba moja kwa siku nyingi sana. Nyumba hiyo pia ilinunuliwa kama sehemu ya uwekezaji wake.

Anawakumbusha wenye kadi za mikopo 'kredit kadi' wanaotumia pesa kwa kadi ya mkopo wanaweza kupunguza matumizi yao kwa kubadili tabia hiyo.

## LAZIMA USHUGHULIKE

Mtaalamu Tracy, anasema maendeleo hayawezekani bila kuwapo na hatua. Anasema wale ambao wanataka kufikia utoshelevu wa kifedha wanapaswa kuendelea na shughuli inayofaa kila wakati na hukua ubaguzi kwa hili.

Mmea hauwezi kukua bila mbegu na bila shughuli za kutafuta fedha hakuna mapato.

Anaeleza jinsi ya kuondokana na deni, akisema kanuni ya msingi ya fedha za binafsi ni kulipa madeni madogo kwanza.

Inasemekana kuwa deni ni kitu kibaya na mara tu unapokwama ndani yake, ni vigumu kutoka na huongeza fedheha.

Anaeleza kuwa si sahihi kuchagua njia potofu kwa mapato ya haraka haraka, kwa mfano, kamari au kubeti, anaonya kuwa kucheza kamari kidogo ni sawa, lakini ukizoea kucheza kamari kwa kiwango kikubwa katika miji kama Las Vegas, maisha yatazidi kwenda juu chini.

Wale wanaofuata maendeleo ya kifedha maishani wanapendekeza kwamba ni muhimu kujiepusha na kucheza kamari, hata hivyo hajasema ni kwa sababu gani.

Soko la hisa na mali ya majengo isiyohamishika pia linazungumziwa na wataalam wa fedha za binafsi wanaosema kurudia kuelewa tofauti kati ya soko la hisa na mali isiyohamishika kama majengo na mashamba ni muhimu.

Malengo tofauti ya kifedha yanapaswa kuamuliwa kwa hayo mambo mawili na kwamba mbinu za uwekezaji zinapaswa kuchaguliwa ipasavyo.

Tracy anapendekeza kufanya maamuzi ya mali isiyohamishika bila hisia, wale wanaowekeza kupitia soko la hisa wanashauriwa kupata faida kutoka kwa fedha za faharisi na kuchukua maamuzi katika mwelekeo huo.

BBC SWAHILI



# Katibu Mkuu CCM aipongeza serikali upatikanaji wa maji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameipongeza serikali kwa kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dodoma.

Chongolo aliyasema hayo hivi karibuni alipokuwa akikagua mradi wa maji Nzuguni unaogharimu Sh. bilioni 4.8 unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA).

Alisema serikali imefanya kazi kubwa katika kutatua tatizo la maji kwa kutekeleza miradi ya maji.

"Kazi kubwa inayofanywa katika kutekeleza miradi ya maji kunatafsiri kuwa mnaelekea kutatua changamoto ya ukosefu wa maji kwa wananchi na kuimarisha uhai wa wananchi, kwa hayo ni muhimu kwa kweli niipongeze sana serikali," alisema.

Naye Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, aliomba serikali kuharakisha ulipaji fidia kwa wananchi ambao wameridhia kupitisha mradi wa maji Nzuguni.

Pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia uchimbaji wa visima pembezoni ikiwamo mradi wa Nzuguni.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, alisema mradi umefika asilimia 74 na unaendelea na ujenzi wa vibanda vya kuendeshea visima, ujenzi wa ofisi ya kuendeshea miradi, kuagiza pampu za kusukumia maji na ujenzi wa misingi ya matangi ya lita milioni 3.5.

Alisema katika ekari 2.7 ya viwanja 58 vilivyoguswa na miundombinu ya maji tayari uthamini umefanyika na watu 24 wanaomiliki viwanja 25 wametambuliwa.

Aidha, alisema Ofisi ya Jiji la Dodoma inaendelea na awamu ya pili ya utambuzi wa wamiliki wa viwanja 33 ambavyo vimebaki.

"Wananchi wote ambao wapo katika eneo la Nzuguni A waendelee na shughuli zao za kuendeleza viwanja wanavyomiliki isipokuwa viwanja 58 tu," alisema.

Mhandisi Joseph alisema utekelezaji wa mradi huo katika Kata ya Nzuguni utanufaisha wakazi 75,968 wa eneo la Nzuguni na maeneo ya jirani ya Ilazo, Swaswa na Nyumba 300 na unatarajiwa kukamilika Agosti mwaka huu.

# Halmashauri zapewa maagizo kuhusu fedha za mradi Boost

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

HALMASHAURI nchini zimeagizwa kukamilisha kwa wakati miundombinu ya shule inayojengwa kwenye maeneo yao kupitia fedha za mradi wa BOOST ili kuvutia mataifa mengine kujifunza uwekezaji wa sekta ya elimu.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Dk. Charles Msonde alitoa agizo hilo jana alipokuwa akikagua miradi ya ujenzi wa shule za msingi na sekondari katika halmashauri za wilaya za Manyoni, Itigi, Ikungi na Singida mkoani Singida.

Alisema kukamilika kwa miundombinu hiyo itafanya Tanzania iwe nchi ya mfano kwa mataifa mengine kuja kujifunza mafanikio ya sekta ya elimu kutokana na kukamilika ujenzi wake.

Msonde alisema halmashauri zihakikishe zinakamilisha miradi ya BOOST ifikapo Julai 30, 2023 ili wanafunzi wajiunge katika shule na kuanza kutumia majengo hayo.

"Tanzania itakuwa nchi ya mfano katika uboreshaji wa miundombinu ya shule na nina amini kwa nchi nyingine za Afrika na mataifa mengine yatakuja kujifunza kuona jinsi tulivyofanikiwa kutokana na kazi kubwa na nzuri aliyoifanya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha nyingi kwenye sekta ya elimu," alisema.

Alisema fedha zilizopokelewa kwa awamu ya kwanza ambazo zimetolewa kama mkopo na Benki ya Dunia (WB) kwa ajili ya kutekeleza mradi huo wa BOOST kwa miaka mitano ni Sh. trilioni 1.15 na umelenga kuimarisha ujifunzaji katika elimu ya awali na msingi.

Dk. Msonde alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne kwenda cha tano na sita hivyo kwa kuwa serikali ni sikivu ikaona ni vema kujenga shule hizo kwa ajili ya wanafunzi hao.

Alizipongeza halmashauri za Manyoni, Ikungi na Singida kwa kuzisimamia vizuri fedha hizo na kutekeleza miradi hiyo kwa viwango na kwa wakati na akahimiza kuongeza kasi zaidi ili ikamilike ndani ya muda uliopangwa.



Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Mkoa wa Dodoma (SHIVYAWATA), Justust Ng'wantalima (kulia), akizungumza na baadhi ya wazee wenye ulemavu wa Kata ya Nkulabi jijini Dodoma jana, akiwasisitizia umuhimu wa kuwapeleka watoto wao shuleni ambao wana ulemavu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watanzania waitwa kuchangia damu kwa wagonjwa selimundu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kujitokeza kwa wingi kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wagonjwa hasa wenye tatizo la selimundu na wajawazito.

Mkuu wa Kitengo cha Damu Salama kutoka Hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa, Kucy Michael alitoa wito huo juzi kwenye uchangiaji damu lililofanywa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya jeshi hilo tangu kuanzishwa.

Alisema hivi sasa Hospitali ya Benjamini Mkapa imeanzisha huduma ya upandikizaji uboho hivyo damu inahitajika kwa wingi ili kuokoa maisha ya wagonjwa wenye tatizo la selimundu pamoja na wajawazito.

"Katika upandikizaji uboho zinahitajika chupa zisizopungua 80 ili kuwahudumia wagonjwa wa matatizo ya selimundu," alisema.

Alieleza kuwa wajawazito pamoja na waathirika wa ajali wanahitaji damu hivyo watu wajitokeze kuchangia damu kwa ajili ya kusaidia wagonjwa mbalimbali.

"Tunawashukuru JKT kwa kujitolea kuchangia damu wamepanga kuchangia chupa 500 tunaomba na taasisi nyingine ziige mfano wa JKT kwa ajili ya kuokoa maisha ya wagonjwa wenye uhitaji wa damu," alisema Michael.

Alifafanua kuwa anawashukuru JKT kwa niaba ya Mkurugenzi wa Hospitali ya Benjamini Mkapa kwa kuwafanya kuwa sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 tangu JKT lianzishwe huku akiwapongeza kwa kujitolea kuchangia damu.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Tiba wa JKT, Meja Yusuf Sasamalo, alisema kwa Dodoma JKT wamejipanga kuchangia chupa 500 za damu na uchangiaji utaendelea katika vikosi vingine vya JKT.

Alisema wameamua kufanya hivyo ili kusaidia wagonjwa mbalimbali wenye uhitaji wa damu na ni moja ya sehemu ya kusherehekea maadhimisho ya miaka 60 ya jeshi hilo tangu lianzishwe hivyo JKT inajitoa kushiriki katika matukio ya kijamii.

Naye Mkuu wa Sheria wa JKT, Kanali Projesteus Rutaihwa, alisema JKT kama sehemu ya jamii wamekuwa wakitembelea maeneo mbalimbali kushiriki usafi pamoja na kutoa misaada katika vituo vya kulelea watoto yatima.



# Kaya zaidi ya 59,000 Mbeya zaongozwa na wanawake

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAYA zaidi ya 59,000 jijini Mbeya zinaongozwa na wanawake kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo wanaume kutelekeza familia, wanawake kuimarika kiuchumi kuliko wanaume.

Mtaalamu wa takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Geve Kasto, aliyasema hayo juzi wakati wa mafunzo maalumu kwa wandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya na wadau wengine kuhusu umuhimu wa matumizi ya takwimu za sensa.

Alisema Jiji la Mbeya lina kaya 154,431 ambazo kati yake ni kaya 94,572 pekee ndizo zenye wanaume ambao ndiyo wakuu wa kaya na zinazobakia zinaongozwa na wanawake.

Alisema mbali na wanawake kutelekezewa familia, pia baadhi ya wanawake ni wakuu wa kaya kutokana na kufiwa na waume ama kutengana na waume zao.

"Kwa hiyo tunaishauri serikali iongeze juhudi za kuwawezesha wanawake kiuchumi ili kuwaimarisha zaidi, sasa hivi imekuwa jambo la kawaida wanawake kuwa wakuu wa kaya," alisema Geve.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema tatizo hilo limesababisha ongezeko la watoto wa mtaani ambao baadhi yao wameanza kuingia kwenye makundi hatarishi wakiwamo wanaotumia dawa za kulevya.

Alisema kutokana na tatizo hilo Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa imeanzisha mikakati maalumu ya kushughulikia tatizo hilo ili kuwanusuru watoto na majanga hayo ambayo yanahatarisha maisha yao.

Homera alisema wapo baadhi ya wanaume wanawazalisha wanawake watoto na kuwatelekeza bila kuwahudumia jambo ambalo linasababisha watoto kulelewa na mzazi mmoja.

Alisema hivi karibuni baadhi ya watoto walikamatwa katika maeneo ya Kabwe na Mwanjelwa jijini Mbeya wakitumia dawa za kulevya.

"Hatuwezi kuwaacha watoto hawa waharibike, tumeanzisha mikakati yetu ya ndani kwa ajili ya kushughulikia jambo hili, kwa sasa hatuwezi kuisema mikakati hiyo lakini muda ukifika tutaiseme," alisema Homera.

Alisema baadhi ya watoto hao wa mitaani wamekuwa wakikamatwa na kupelekwa mahabusu lakini ndugu zao hawajitokezi kwenda kuwachukua na kwamba hata waliochukuliwa na ndugu zao bado wanarudi tena mtaani.

Alisema baada ya kukamilisha mikakati hiyo wataanza kuwakamata na kuwachukulia hatua ikiwamo kuwapeleka kwenye mahakama za watoto ili iwe funzo kwao.

Mtakwimu kutoka NBS, Mariam Kitenge, alisema kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka jana Mkoa wa Mbeya una zaidi ya watu milioni 2.3 huku Jiji la Mbeya pekee likiwa na watu 500,000.

Alisema takwimu hizo zinaonyesha kuna ongezeko kubwa la watu kwa maelezo kuwa sensa ya mwaka 2012 Mkoa wa Mbeya ulikuwa na watu milioni 1.7.

Alisema sensa ina maana kubwa kwa maendeleo ya taifa ikiwamo kuvutia wawekezaji ambao huwa wanataka kujua idadi ya watu kenye eneo wanalotaka kuwekeza kulingana na mahitaji yao.

Aliwataka waandishi wa habari na wadau mbalimbali kuzitumia takwimu hizo kwenye shughuli zao ili kuchochea maendeleo ya taifa.



Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo (kushoto), akimkabidhi tuzo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, kutokana na msaada alioutoa wakati katika uanzishwaji wa Taasisi ya Suma Ikenda Foundation kwenye uzinduzi wa taasisi hiyo, mwishoni mwa wiki. **PICHA NEBART MSOKWA**

# Wananchi walalamika nyumba zao kuvamiwa na wachimbaji

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

WAKAZI wa Kitongoji cha Kibaoni Kata ya Saza wilayani Songwe, wamewalalamikia baadhi ya wachimbaji wa madini katika eneo hilo wakidai kuwa wanachimba mpaka kwenye makazi yao hali ambayo inahatarisha maisha.

Wamesema wachimbaji hao wamekuwa wakichimba dhahabu na kuacha mashimo ambayo yanahatarisha nyumba zao kubomoka pamoja na maisha yao kuwa hatarini endapo nyumba hizo zitabomoka wakiwamo.

Wameiomba serikali kuingilia kati kuwazuia watu hao kwa maelezo kuwa kwa sasa hali imekuwa mbaya na wamekuwa wakiwatishia maisha wanapowazuia kufanya shughuli hizo.

Wakizungumza na Nipashe kwa masharti ya kutotajwa majina yao ili kulinda usalama wao kwa sababu ya vitisho wanavyovipata wananchi walisema hali imekuwa mbaya na huenda wakapoteza makazi yao.

Mmoja wa wakazi hao alisema baadhi ya nyumba zao zimeanza kubomoka na nyingine kupata nyufa kutokana na mtikisiko unaotokana na uchimbaji unaoendelea kwenye maeneo hayo.

Alisema wachimbaji hao wamekuwa wakijinasibu kuwa hakuna mtu mwenye uwezo wa kuwazuia kufanya shughuli zao kwenye eneo hilo jambo ambalo linazidisha zaidi hofu.

"Tunajiuliza nyumba zetu zikibomoka tutaishi wapi na familia, tukihoji tunapewa vitisho, hali imekuwa mbaya na tunaishi kwa hofu, tunaiomba serikali iingilie kati kuwazuia wachimbaji hawa ili tuishi kwa amani," alisema mwananchi huyo.

Alisema walishawasilisha malalamiko kwa maandishi katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Mei 12 mwaka huu pamoja na ofisi ya Ofisa Madini Mkazi Aprili 27 lakini bado tatizo linaendelea na hakuna hatua zilizochukuliwa.

Mwananchi mwingine alisema wanaogopa kulalamika hadharani wala kuandamana kwa sababu ya kuhofia usalama wao kutokana na kutishiwa mara kwa mara na vikundi vya wachimbaji hao.

Alisema kwa sasa hawana amani ya kuendelea kuishi kwenye eneo hilo kutokana na vitisho ambavyo wamekuwa wakipata kutoka kwa wachimbaji.

Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Solomon Itunda, alikana kupokea malalamiko ya wananchi hao huku akikiri kuwa Kata ya Saza ni miongoni mwa kata za uchimbaji wa madini ya dhahabu.

Alisema kama taarifa ya tatizo hilo iliwasilishwa ofisini kwake huenda ilikuwa kipindi cha nyuma kabla yeye hajawa mkuu wa wilaya hiyo. Aliahidi kufuatilia jambo hilo kwa kufanya ziara kwenye eneo hilo ili kujiridhisha kabla ya kuanza kulishughulikia na kwamba atalitatua bila kuumiza upande wowote.

"Naahidi kulifuatilia ili kujiridhisha na kulifanyia kazi, hata ofisi ya ofisa madini iko chini yangu nitafuatilia na nitalimaliza kwa usalama," alisema Itunda.

Alisema hakuna mtu yeyote ambaye yuko juu ya sheria na hivyo akawataka wanaotishiwa kwenda ofisini kwake kuwasilisha taarifa hizo kwa siri ili serikali ichukuwe hatua dhidi ya wanaotishia.

# Wadau waitwa kushirikiana na serikali mapambano udumavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU mkoani Mbeya wamehimizwa kuungana na serikali kupambana na hali ya udumavu hususani kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano kwa kushiriki kampeni mbalimbali za kuiwezesha jamii kutambua umuhimu wa lishe bora na upatikanaji wake.

Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa 12 nchini iliyotajwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwa mkoani Mtwara wakati wa kuwasha Mwenge wa Uhuru kuwa na kiwango kikubwa cha udumavu kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Alisema mkoa huo ni miongoni mwa mikoa yenye kiwango cha juu na kwamba kwa sasa Mbeya ina kiwango cha asilimia 31.5 ambacho nni juu ya wastani wa kitaifa na aliwataka wakuu wa mikoa husika kuitafakari hatua hiyo na kuchukua hatua stahiki.

Katika kikao maalumu cha kujadili utekelezaji wa lishe katika Jiji la Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwataka wadau wote kuungana na serikali ili kukabiliana na tatizo hilo ambalo linachafua taswila ya mkoa.

Miongoni mwa wadau aliosema ni muhimu kushiriki kwenye mapambano hayo ya udumavu ni pamoja na mashirika binafsi yanayojishughulisha na masuala ya kijamii ikiwamo afya na uchumi imara pamoja na taasisi zinazojikita kwenye shughuli za uzalishaji.

"Katika kuepuka hali ya udumavu kwa watoto wetu, kama alivyojitokeza hapa mdau wetu WeCare Foundation basi tuwahamasishe na wadau wengine huko waliko washirikiane na sisi ili kutimiza lengo la serikali katika kuhakikisha watoto wanakuwa katika makuzi salama na yenye lishe bora," alisisitiza Malisa.

Aliwapongeza watendaji wa halmashauri na wadau wengine kwa kuanzisha mikakati ya kusaidia jamii maeneo ambayo serikali ilinakuwa imekwama ama inaendelea.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa wa shughuli za WeCare Foundation, Mkurugenzi mwasisi wa shirika hilo, Elizabeth Maginga alisema katika kuimarisha malezi na makuzi ya awali ya mtoto wanashirikiana na wadau wengine wanaojihusisha na shughuli za kijamii zinazotoa huduma kwa watoto.

Alisema baada ya kufungua kituo cha mafunzo ya malezi na makuzi ya awali ya mtoto kwa wazazi na walezi katika Kituo cha Afya cha Aghakan cha jijini Mbeya taasisi hiyo ina mpango wa kutoa huduma kama hiyo katika Hospitali ya Kanda ya Mbeya Kitengo cha Wazazi na Watoto cha Meta.



## Kampuni ya SGA yaahidi kuendeleza ushirikiano na polisi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya ulinzi ya SGA imeahidi kuendeleza utamaduni wake wa mahusiano ya karibu wa kikazi na Jeshi la Polisi Tanzania.

Ahadi hiyo imetolewa mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya kuwakumbuka waasisi wa kampuni hiyo, marehemu Philemon Mgaya na marehemu Edmond Tongeren kutoka Uholanzi ambao walianzisha kampuni hiyo mwaka 1984.

Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Security, Eric Sambu, alisema kampuni hiyo sasa inaajiri zaidi ya wafanyakazi 5,000, kwamba idadi hiyo imeanza kuongezeka baada ya kushuka hivi karibuni kutokana na ongezeko la ghafla la kima cha chini cha mishahara kulikosababisha baadhi ya wateja kutafuta huduma zingine za bei nafuu.

"Tumepitia mengi lakini kila tunapokumbana na changamoto huwa tunakabiliana nazo na kupata mafanikio makubwa," alisema Sambu.

Alisema siri ya mafanikio ya kampuni hiyo ni ushirikiano mzuri ulionao uongozi na wadau muhimu katika biashara jambo ambalo alisema ni utendaji mzuri wa kampuni hiyo.

Aidha, alisema katika hafla hiyo, pia waliwatunukia zawadi mbalimbali watumishi wa kampuni hiyo waliofikiwa umri wa kustaafu.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na wafanyakazi walioitumikia kampuni hiyo kwa zaidi ya miaka 20, ambapo walipata fursa ya kujiunga na klabu maalum ya kampuni hiyo ijulikanayo kama klabu 20, ambayo inahusisha zaidi ya wafanyakazi 200 wa kampuni hiyo ambao tayari washaitumikia kwa miaka 20 maeneo mbalimbali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, ACP Mtatiro Kitinkwi, aliupongeza uongozi wa Kampuni ya SGA Security kwa kuwa mshirika wa karibu wa serikali kupitia Jeshi la Polisi nchini.

Akitoa mfano wa ushirikiano baina ya taasisi hizo mbili, ACP Mtatiro alisema ni ushirikiano ambao SGA Security hutoa kupitia doria hususani mwishoni mwa wiki.

Alitoa wito kwa kampuni zingine za ulinzi kuiga mfano mzuri wa utendaji bora wa shughuli za ulinzi unaofanywa na Kampuni ya SGA Security.

Pia, aliipongeza Kampuni ya SGA Security kwa kujali maslahi ya wafanyakazi walioajiriwa na kampuni hiyo ikiwamo kuwatunukia.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Kampuni za Ulinzi za Binafsi nchini (TUPSE), Charles Basondole, alitoa shukrani kwa uongozi wa SGA Security kwa kujali maslahi ya wafanyakazi.

Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya SGA, Oscar Mgaya alilishukuru Jeshi la Polisi kwa ushirikiano wa karibu inaotoa kwa kampuni hiyo.

# Mariam Mwinyi: Kuna wimbi la mmomonyoko wa maadili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi amesema kuna wimbi kubwa la mmomonyoko wa maadili ambayo yamechangia kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji na kuleta athari kwa taifa.

Aliyasema hayo visiwani humo katika hotuba yake iliyosomwa na Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma wakati akifungua mkutano mkuu wa pili wa Jumuiya ya Wanawake Wamiliki wa Shule Binafsi na Vyuo vya Elimu ya Kati Tanzania na Zanzibar.

Aliwataka wamiliki wa shule na vyuo binafsi vya kati kujikita katika kuwapatia stadi za maisha watoto ambazo zitawasaidia kujilinda na matukio ya udhalilishaji wa kijinsia ambayo hurudisha nyuma ndoto zao katika elimu.

Alisema hivi sasa kumejitokeza wimbi la matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ambayo kwa kiasi kikubwa vimechangiwa na kuporomoka kwa maadili katika jamii.

Mgeni alisema katika matukio hayo miongoni mwa waathirika wake wakubwa ni wanafunzi wa kike ambao hukabiliwa na mambo mengi ikiwamo mimba na hivyo kutishia kukatisha ndoto zao katika elimu.

Aidha, alisema wanafunzi wa kike wanatakiwa kupewa elimu ya kujilinda na kufahamu viashiria vyote ikiwamo vishawishi vinavyoweza kusababisha kupeleka udhalilishaji wa kijinsia katika jamii.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdul Gulam Hussein, alisema Wizara ya Elimu kwa upande wa Zanzibar inafurahishwa kuona idadi ya wamiliki binafsi wa shule wanaongezeka hatua ambayo imefunguwa fursa za elimu kwa watoto.

Alisema uwekezaji wa sekta ya elimu ndiyo kipaumbele cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi kupata elimu katika kiwango cha juu.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wamiliki wa Shule na Vyuo vya Kati Binafsi, Yustin James alisema wanajivunia mafanikio makubwa tangu taasisi hiyo kupata usajili wake na kuanza kazi mwaka jana huku asasi zaidi ya 200 zikijiunga na umoja huo.

Aidha, alisema umoja huo unaonesha malengo ya wanawake kwamba wanaweza bila ya kuwezeshwa kwa sababu unaundwa kwa asilimia 90 na wanawake wamiliki wa shule na vyuo vya kati nchini Tanzania.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (kulia), akizungumza na Balozi wa Tanzania nchini Uturuki, Balozi Idd Seif Bakari, alipofika ofisini kwa makamu kwa ajili ya kumuaga kwenda kituo chake cha kazi. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS**

# Wizara ya Fedha yaagizwa kujipanga malipo ya pensheni wazee

**Na Mwandishi Wetu**

OFISA Mdhamini wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Pemba, Shuweikh Abdallah Omar, amewataka watendaji wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Pemba kujipanga kufanya maandalizi ya mapema ya malipo pensheni jamii ya wazee kufuatia mabadiliko yaliyofanywa katika Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023-2024.

Alisema hayo alipokutana na watendaji wa Ofisi ya Wizara ya Fedha na Mipango Pemba pamoja na Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kuweka mikakati na kuanza kutayarisha malipo ya pensheni kwa wazee waliofikisha umri wa miaka 70.

Alisema serikali tayari imetangaza nyongeza ya asilimia 150 ya pensheni ya jamii kwa wazee waliofikisha umri wa miaka 70 inayotarajiwa kuanza kutekelezwa Julai mwaka huu.

Alisema Rais Hussein Ali Mwinyi tayari ametoa agizo la kuanza wastaafu kulipwa pensheni jamii kwa nyongeza ya asilimia 150 ambayo ni kutoka Sh. 20,000 walizokuwa wakipokea hadi Sh. 50,000 kwa mwezi.

Alisema agizo hilo linatakiwa litekelezwe kwa sababu tayari limepitishwa katika bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2023-2024 na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya.

## Umoja wa Falme za Kiarabu kuzijengea uwezo manispaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UBALOZI mdogo wa Umoja wa Falme za Kiarabu Zanzibar umeahidi kuzijengea uwezo manispaa Zanzibar kwa ajili ya kusimamia majukumu yake ikiwamo kubuni miradi ya kiuchumi.

Hayo yalisemwa na Balozi Mdogo wa Umoja wa Falme za Kiarabu Zanzibar, Saleh Ahmed Al-Hemeir, wakati alipofanya mazungumzo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Idara Maalum SMZ, Masoud Ali Mohamed.

Alisema Umoja wa Falme za Kiarabu kupitia manispaa zake zimepiga hatua kubwa ikiwamo kubuni miradi ya kiuchumi, usafi wa miji pamoja na kutoa huduma za kijamii.

Aidha, alisema miongoni mwa majukumu ya manispaa za miji katika Umoja wa Falme za Kiarabu ni pamoja na kubuni huduma za afya na elimu pamoja na ujenzi wa shule.

Alisema Umoja wa Falme za Kiarabu utatoa nafasi ya ziara kwa watendaji wa manispaa ya miji ya Zanzibar kujifunza hatua ambayo itawawezesha kuwa wabunifu zaidi katika miradi ya maendeleo na kiuchumi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum, Masoud Ali Mohamed, alisema Serikali ya Zanzibar imefarijika kitendo cha umoja huo kufungua ubalozi wake nchini ambapo ni fursa nyingine kwa Zanzibar kupiga hatua kubwa za maendeleo.

Alisema Zanzibar imejipanga kuimarisha manispaa zake Unguja na Pemba kuona zinajiendesha kimapato katika ukusanyaji wa kodi ambapo watendaji wake wanahitaji kupatiwa utaalamu zaidi katika eneo hilo.

Aidha, alisema manispaa za Zanzibar zinahitaji kujengewa uwezo katika ubunifu ikiwamo katika miradi ambayo itatumika kiuchumi na maendeleo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KEVIN SAWAYA MUSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 608 AVE – MITSUBISH PICK UP.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/227014/2023.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 113 LA 2023**
**ALEX VICTOR WAYSON...MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
- **FOUNDATION SCHOOL LTD**
- **PAMELA BHANJI......MDAIWA/WADAIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**
- **FOUNDATION SCHOOL LIMITED**
- **PAMELA BHANJI – POPOTE ULIPO/MLIPO**

ALEX VICTOR WAYSON amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/tarehe 20/7/2023 saa 3:00 Asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 20 Mwezi wa 06 Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

### KIWANJA KINAUZWA

**KIWANJA KIPO KISUKURU** SEGEREA **JKT DSM,** KINA UKUBWA WA MITA ZA MRABA **(SQM) 2252,** KIWANJA KIMEPIMWA KINA HATI, **BEI MILIONI 60.** KWA MAWASILIANO: **0754 857523, 0655857523**

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MODEV ENTERPRISES CO LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA **SANLG** YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC197DQB.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI **BGA/TR /RB/1125/2023**

### KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**KASSIM MOHAMED NINDI** WA WILAYA YA NAMTUMBO - RUVUMA Anatangaza Kupotea kwa Kadi ya **TREKTA - SONALIKA ,HP 45 PL.NO ,T 922 D.E.H** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi .
TAARIFA YA POLISI : **NT/RB/ 440/2023.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KEVIN SAWAYA MUSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 608 AVE – MITSUBISH PICK UP.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/227014/2023.**

### KUPOTEA KWA CHETI



**ANNA CHRISTOPHER** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo chenye usajili namba: **0066/T.2007** kilichotolewa na CHUO CHA ARDHI mwaka 2011. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/OST/RB/231041/2023**

### KUPOTEA KWA PASSPORT



**NJAMA AZIZI ALLY** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE239216** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 11/11/2019. Yeyotea atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/KIL/RB/231612/2023.**

### KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**BARAKA AIYONA MATERU** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE USAJILI WA JINA **MACLINA KABIRA,** NAMBA **MC119 BLH ,** CHASIS **NO:MD6M14PK9G4F23397,** ENGINE NO: **OK4FG4035554.** YEYOTE ATAKAYEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU YAKE JALADA NAMBA **IRI/IRI/RB/231329/2023.**

### KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MOHAMEDI JUMA BAKARI** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya **BAJAJI** (tvs bajaji) yenye namba za usajili **MC 229 DNC,** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi kilichokaribu yake.
**MOR/MOR/RB/187044/2023**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA CHATO**
**KITUO CHA CHATO MJINI**
**SHAURI LA MADAI NA. 55 LA 2023**
**DAUD EMMANUEL MANYAMA..........MDAI**
**DHIDI YA**
**PROCHESPROSPER TEGAMAISHO...MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

MDAI AMELETA MAOMBI YA KUKAZA HUKUMU ILI KULIPWA 4,181,000 TSHS KATIKA MAHAKAMA MNAMO TAREHE 11/07/2023 SAA 2.30 ASUBUHI NA UNATAKIWA KUWEPO, AU KUWAKILISHWA KISHERIA PAMOJA NA KULETA UTETEZI WAKO DHIDI YA MAOMBI HAYA.
ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWAKO TAREHE HIYO, SHAURI LITAANZA KUSIKLIZWA BILA WEWE KUTAARIFIWA TENA NA MAAMUZI KUTOLEWA.
IMETOLEWA KWA MKONO WANGU NA MHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 04/07/2023.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
CHATO MJINI

**NYADHI INVESTMENT Co. LTD**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**M/MWANZO ILEMELA - SHAURI LA MADAI YA TALAKA NA. 121/2022**
**ANNASTAZIA MARWA WANGWE.........MDAI MUHUKUMIWA**
**DHIDI YA**
**KENNEDY MWITA GIMUGE.........MDAIWA MUHUKUMIWA**

KWA IDHINI YA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAYO NI NYUMBA MOJA (1). MNADA UTAFANYIKA MAHALI MALI ILIPO. NYUMBA NA. 09 ILIYOPO TANKI LA MAJI, KATA YA NYASAKA, WILAYA YA ILEMELA. MNADA UTAFANYIKA TAREHE 10/08/2023 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA.

**MASHARTI YA MNADA:**
1. KWA MALI INAYOHAMISHIKA, MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI
2. KWA MALI ISIYOHAMISHIKA, MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI

**MAWASILIANO : 0768-588155**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: ANJAM ISMAIL ATHUMANI wa SABASABA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA DOTTO ATHUMANI**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 19 Mwezi 07 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 05 mwezi 07 mwaka 2023**

G. A. MRISHO
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMISTRATION CAUSE NO...18....OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GERALD MOZAN MAPEMBE**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LATER OF ADMINISTRATION**

**BY RASHID AUGUSTINO MAPEMBE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be field on or before the 24 day of July 2023
Dated at Korogwe this 21 day of June 2023.

DISTRICT COURT
KOROGWE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE DISTRICT

**OFISI ZA MATANGAZO**
*Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.*
*Mobile: +255 - 745 700 710.*
*E-mail: advertise@guardian.co.tz,*
*Website: www.ippmedia.com*

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA



Wafuasi wa kiongozi wa upinzani nchini Kenya, Laila Odinga, wakitawanywa kwa kutumia mabomu ya machozi hivi karibuni. Jeshi la Polisi nchini humo limeshutumiwa kwa matumizi ya nguvu kupita kiasi dhidi ya waandamanaji. **PICHA: REUTERS**

# Putin akutana na Prigozhin Ikulu

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, amekutana na kiongozi wa kundi la mamluki la Wagner, Yevgeny Prigozhin, siku chache baada ya kushindwa kwa jaribio la uasi.

Kulingana na msemaji wa Ikulu ya Kremlin, Dmitry Peskov, kiongozi huyo wa Wagner alikuwa miongoni mwa watu 35 walioalikwa kwenye mkutano huo mjini Moscow, uliofanyika hivi karibuni.

Alisema kuwa Rais Putin alitoa tathmini ya juhudi zinazoendelea katika vita vya Ukraine na uasi uliotokea.

Uasi huo uliofanyika Juni 23 na ulidumu kwa saa 24 pekee.

Chini ya makubaliano ya kumaliza mzozo huo, mashtaka dhidi ya Prigozhin yalifutwa na akapewa chaguo la kuhamia Belarusi.

Kumekuwa na majibizano ya hadharani kati ya Wagner na Wizara ya Ulinzi ya Russia kuhusu mwenendo wa vita hivyo. Prigozhin alikuwa ameishutumu wizara mara kwa mara kwa kushindwa kulipatia kundi lake risasi.

Akizungumza jana, Peskov alisema mkuu huyo wa Wagner alikuwa miongoni mwa makamanda walioalikwa Kremlin siku tano baada ya maasi hayo.

"Rais alitoa tathmini ya hatua za kampuni hiyo katika mstari wa mbele," alisema Peskov wakati akihojiwa na shirika la habari la Interfax.

Aliongeza, "Pia alitoa tathmini kwa matukio ya Juni 24. Putin alisikiliza maelezo ya makamanda na kupendekeza njia tofauti za ajira zao za baadaye na matumizi yao ya baadaye katika vita."

Kulingana na msemaji huyo, Prigozhin alimwambia Putin kwamba Wagner inamuunga mkono bila masharti.

Wakati huo huo, hofu ya uwepo wa mamluki kutoka kundi la Wagner kutoka Russia na kuhamia Belarus kama sehemu ya makubaliano yaliyofikiwa kumaliza uasi, umesababisha Poland kuweka tayari vikosi vya kijeshi mpakani.

Hatua nyingine iliyochukuliwa ni mpaka uliowekwa alama kwa nguzo za mbao tayari umebadilishwa kwa kuwekwa uzio wa chuma ikiambatana na kamera za kisasa na vifaa vingine vya ulinzi.

Nguzo hizo ziliwekwa baada ya Belarus kuanza kuhimiza maelfu ya wahamiaji kuvuka hadi Poland miaka miwili iliyopita.

Kabla ya mkutano wa kilele wa Nato wa wiki hii nchini Lithuania, serikali ya Poland imekuwa ikionya kwamba vikosi vya Wagner vinaweza kutumika kuzua matatizo zaidi, kwa hivyo inapeleka mamia ya wanajeshi wa ziada katika mpaka wake wa mashariki kama tahadhari.

"Tishio kubwa zaidi ni kwamba jirani yetu, Belarus, haitabiriki kabisa," alisema Michal Bura.

"Tunapaswa kuwa tayari kwa hatua yoyote. Labda Wagner watakuwa tatizo, lakini hakuna anayejua kwa nini wanaenda huko au wanajiandaa kwa ajili gani," aliongeza.

Makubaliano ya haraka yalikusudiwa kuzuia mapigano na wapiganaji wake wa Wagner kuhamishwa hadi Belarusi na kiongozi wao.

Lakini kambi kubwa ya hema nje ya Minsk, ambayo huenda imetayarishwa kwa ajili yao, inaleta wasiwasi kwa Poland kuwa ni kwa ajili ya kundi hilo ambao askari wake wameonakana.

**BBC**.



## Marekani yazidi kupingwa mabomu ya Cluster

**WASHINGTON,** MAREKANI

NCHI washirika wa Marekani wamezidi kusikitishwa na uamuzi wa serikali ya Marekani, kusaidia kuwasilisha mabomu ya Cluster nchini Ukraine.

Marekani ilithibitisha Ijumaa iliyopita kwamba itatuma mabomu hayo yenye utata nchini Ukraine na Rais Joe Biden akiuelezea uamuzi huo kuwa mgumu.

Katika kukabiliana na hilo, Uingereza, Canada, New Zealand na Uhispania pia zimezungumza dhidi ya matumizi ya silaha hiyo.

Zaidi ya nchi 100 zimepiga marufuku utumiaji wa mabomu ya vishada kwa sababu ya hatari zinazowakabili raia.

Mabomu haya yanatoa mabomu mengine madogo ambayo yanaweza kuua watu katika maeneo ya jirani.

Aidha, mabomu ambayo hayajalipuka yanaweza kuishi muda mrefu na kisha kulipuka baada ya kukanyagwa au kuguswa na watu.

Rais Biden alisema kwamba ilimchukua muda mrefu kufanya uamuzi huu na pia alisema kuwa `Waukraine wanaishiwa na risasi.'

Uamuzi huu umekosolewa na mashirika ya kutetea haki za binadamu bila kusita na Amnesty International imesema kuwa mabomu ya makundi yanatishia maisha ya raia kwa muda mrefu baada ya kumalizika kwa vita. **BBC**

# Ali Bongo kuwani tena urais Gabon

**LIBREVILLE,** GABON

RAIS wa Gabon, Ali Bongo Ondimba, ametangaza kuwania muhula wa tatu wa madaraka katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Agosti 26, mwaka huu.

Akitangaza azma yake, Rais Bongo alisema ana ndoto ya kuibadilisha Gabon.

"Tutaifanya na tunaweza kuifanya Gabon kuwa taifa imara, taifa bora, sehemu bora ya kuishi. Hii ni azma yangu, azma ambayo haijashindwa kunisukuma na inaendelea kunipa msukumo kila siku," alisema.

Aliongeza kwamba anaweza kukosolewa kwa mengi lakini sio kukosa ari na ndoto kwa ajili ya taifa hilo.

"Mnanifahamu, kutowezekana sio neno nilijualo. Haijawahi kuwa." Alisisitiza.

Uchaguzi uliopita uliofanyika 2016 ulikumbwa na madai ya udanganyifu wa kura ambapo Rais Bongo alimshinda aliyekuwa mwenyekiti wa Umoja wa Afrika Jean Ping kwa kura zisizozidi elfu sita.

Kiongozi huyo wa Gabon anashutumiwa kwa kuukandamiza upinzani.

Kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 64 alichukua madaraka mwaka 2009 kutoka kwa babake Omar Bongo ambaye aliiongoza Gabon kwa zaidi ya miaka arobaini tangu mwaka 1967 hadi alipofariki dunia.

Gabon haina ukomo wa mihula kuambatana na katiba ya taifa hilo lenye utajiri wa mafuta.

**BBC**

HABARI MICHEZO

# SINGIDA FG YAANIKA MALENGO LIGI KUU BARA, MICHUANO CAF

**Na Saada Akida**

KLABU ya Singida Fountain Gate, imeweka wazi malengo yao kuelekea msimu ujao wa michuano yote watakayoshiriki msimu wa 2023/24, huku ikishindwa kukunjua makucha yao katika suala zima la kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Singida Fountain Gate FC, katika msimu wa 2022/23, ilifanya vizuri kwa kumaliza nafasi ya tatu katika Ligi Kuu hivyo kukata tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Singida Fountain Gate FC, Hassan Masanza, alisema malengo yao ya awali ni kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri katika kila mashindano wanayoshiriki ikiwamo kumaliza nafasi tatu za juu kwenye ligi. Alisema kwenye mashindano mingine ikiwamo Ngao ya Jamii, Kombe la Shirikisho la TFF (FA Cup), Kombe la Mapinduzi linalofanyika kila mwaka visiwani Zanzibar, wanahitaji kufika fainali na michuano ya kimataifa kutinga hatua ya makundi.

"Malengo yetu ya chini ambayo klabu yetu imeyaweka kwa msimu wa 2023/24, matarajio yetu tutafikia malengo hayo kwa asilimia 100 kama tulivyofikia msimu wa 2022/23.

"Matumaini yetu makubwa ni kufikia malengo hayo na ninaimani tutafika kwa kuwa tumefanya usajili mzuri kulingana na mahitaji ya timu kwa kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Hans van Pluijm," alisema Masanza.

Wakati bado mchakato wa kuimarisha kikosi cha timu hiyo ukiendelea, timu hiyo imeingia kambini leo jijini Arusha kikiwa huko kitapata michezo miwili ya kirafiki na timu mbili kutoka nje ya Tanzania, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya msimu ujao, na mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Simba.

Hadi sasa Singida Fountain Gate FC imetangaza usajili mpya ambao ni Yahya Mbegu kutoka Ihefu FC na beki wa Simba, Joash Onyango aliyejiunga na timu hiyo kwa mkopo wa msimu mmoja.




Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya NBC, Elvis Ndunguru (kulia) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa, Nyakaho Mahemba (kushoto), wakionyesha nakala za mkataba utakaowezesha wasanii na wadau wengine kwenye sekta ya sanaa na utamaduni kukopeshwa kwa masharti nafuu na benki hiyo muda mfupi baada ya pande hizo mbili kutiliana saini jijini Dodoma jana. **MPIGAPICHA WETU**

# NBC, Wizara kuwainua wasanii kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imesaini mkataba wa makubaliano na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa, utakaoiwezesha benki hiyo kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wasanii pamoja na kazi za sanaa na utamaduni nchini.

Kwa mujibu wa mkataba huo, wasanii wataweza kukopa hadi Sh. milioni 100 huku riba katika mikopo itakayotolewa chini ya utaratibu huo ikiwa ni asilimia tisa tu, hadi kipindi cha miaka miwili.

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji sahihi mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Biashara wa NBC, Elvis Ndunguru, alisema mkataba huo unaeleza kuwa, wasanii wataweza kupata mikopo ya aina mbili, kwanza kwa ajili ya uwekezaji na pili kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao za kibiashara.

Alisema mikopo ya uwekezaji itawawezesha wasanii kununua vifaa pamoja na kupata mitaji na kwamba utawawezesha wasanii kuwa na vifaa vya kisasa katika kazi zao na hivyo kupanua wigo wa biashara zao.

Ndunguru alisema mikopo ya uendeshaji itasaidia kuwapatia fedha zinazohitajika katika shughuli zao za kibiashara za kila siku.

Aidha, alisema pamoja na mikopo hiyo ya riba nafuu, NBC itatoa elimu ya biashara na fedha kupitia Club za NBC Biashara.

Alifafanua kuwa elimu itakayotolewa itawasaidia kutoa ujuzi wa namna ya kutunza fedha na pia kufanya maamuzi sahihi wanapotaka kuwekeza. Huduma nyingine watakazonufaika nazo wasanii ni pamoja na bima aina mbalimbali, fursa za masoko na ushauri wa kifedha.

"Benki ya NBC inayofuraha kuunganana na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuwawezesha wasanii wetu kupitia mikopo na elimu.

"Mkataba huu ni mwanzo wa kuliwezesha kundi hili muhimu ambalo kwa kipindi kirefu liliachwa nyuma kwenye huduma za kifedha na mikopo. Kwa kuwapatia mikopo yenye riba nafuu pamoja na elimu ya fedha, tutakuwa tumewasaidia kupiga hatua kiuchumi na kuendeleza sekta ya sanaa na utamaduni kwa upana wake," alisema.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pindi Chana, aliishukuru NBC kwa kukubali kutoa mikopo kwa wasanii na kusema kuwa hatua hiyo itasaidia kukuza sekta ya sanaa na utamaduni nchini.

"Napenda kuishukuru NBC kupitia mkataba huu, wasanii wetu hawatapata tena shinda ya mitaji kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao na pia wataweza kukuza biasahara zao," alisema.

Waziri huyo alisema mtandao mpana wa matawi wa NBC ulioenea nchi nzima utawezesha wasanii kunufaika na huduma hii ya mikopo na elimu popote pale walipo.

Ushirikiano huu kati ya NBC na Wizara, ni sehemu ya mkakati wa NBC kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi kupitia huduma za kifedha kwa kuyafikia makundi mbalimbali na kuyapatia huduma kulingana na mahitaji yao mahususi.

## Azam U-17 yazidi kutisha Ligi ya TFF

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kaka zao wakitolewa hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), chini ya miaka 20 hivi karibuni, timu ya Azam FC ya vijana chini ya miaka 17 imeendelea kuongoza na kuziburuza zingine 15 kwenye Ligi hiyo inayoendelea kutimua vumbi Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Vijana hao wanaongoza wakiwa na pointi 28 kwa michezo 10 ambayo wamecheza.

Timu hiyo imeshinda mechi tisa na kutoka sare moja, haijapoteza, huku ikipachika jumla ya mabao 30 mpaka sasa.

Inafuatiwa na Yanga ambao imejikusanyia pointi 26 mpaka sasa, ikicheza michezo 10, kushinda minane, sare mbili ikifunga jumla ya mabao 32.

Nafasi ya tatu inashikiliwa na Ihefu FC ikiwa na pointi 23, yenyewe ikicheza mechi 10, ikishinda michezo saba, sare mbili na kupoteza moja, Simba ikishinda nafasi ya nne kwa pointi 21, ikishinda mechi sita, sare tatu na kupoteza mchezo mmoja mpaka sasa.

Nafasi ya tano inashikiliwa na Mbeya Kwanza na pointi zake 20, Singida Fountain Gate ya sita ikiwa pia na pointi 20, ya saba ni African Sport yenye pointi 15, na iliyo katika nafasi ya nane ni Ruvu Shooting iliyojikusanyia pointi 14.

## China yatoa mil. 100/- vifaa vya michezo

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Dk. Pindi Chana, amepokea vifaa vya michezo vyenye thamani ya Sh. milioni 100 ikiwamo jumla ya mipira 1,800 na jezi 2,634 kutoka Ubalozi wa China nchini.

Vifaa hivyo ni sehemu ya kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na China kupitia sekta ya michezo, ambapo kwa kutoa mipira kwa kila mchezo, soka, netiboli na mpira wa kikapu.

Akizungumza Dar es Salaam jana, katika mapokezi ya vifaa hivyo, waziri huyo alisema ziara za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan nje ya nchi zimeaza kuzaa matunda kwa kuendelea kupata ushirikiano kutoka kwa mabalozi wa mataifa mbalimbali ikiwamo China.

Alisema vifaa hivyo vya michezo watavigawa kwenye shule za mikoa 31, kuendeleza na kuinua michezo kuanzia ngazi ya shule ili kupata wachezaji wazuri wa baadaye kwa manufaa ya timu za taifa.

"Tutaendelea kuhakikisha utamaduni, sanaa na michezo inaendelea kusonga mbele, kuboresha masuala ya michezo, tunataka kupeleka michezo kwa kila mtaa, ngazi za vijiji na kila kata, na kuendelea kusisitiza maeneo ya wazi kulindwa," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TIMBER SAFI ARSENAL

MLINZI wa Uholanzi, Jurrien Timber mwenye umri wa miaka 22, amefanyiwa vipimo vya afya na Arsenal na kurejea nyumbani kwa ajili ya kuaga wenzie kabla ya kukamilisha uhamisho wake kutoka Ajax. **(Metro)**

### VLAHOVIC ATAKIWA CHELSEA

JUVENTUS imeiambia Chelsea kuwa inaweza kumpata mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 23, kwa kutoa euro milioni 25 pamoja na mshambuliaji wao wa Ubelgiji, Romelu Lukaku. **(Corriere dello Sport, via Football London)**

### GERRARD AMTAKA ZAHA

KOCHA mpya wa Al-Ettifaq, Steven Gerrard amefanya mazungumzo na winga wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, kuhusu uhamisho wa pauni milioni 16 kwa mwaka kwenda Saudi Arabia, huku mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 na Crystal Palace ukimalizika. **(Mail)**

### HOJLUND AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inajiandaa kuwasilisha ofa mpya kwa Atalanta kwa ajili ya Rasmus Hojlund, wakiwa tayari wameafikiana kimsingi na mshambuliaji huyo wa Denmark mwenye umri wa miaka 20. **(Nicolo Schira)**

### DEST ATAKIWA PALACE

KLABU ya Fulham na Crystal Palace zina nia ya kumsajili beki wa pembeni wa Marekani, Sergino Dest mwenye umri wa miaka 22, kutoka Barcelona. **(Mundo Deportivo)**

### VEN KUBAKISHWA WOLFSBURG

KLABU ya Wolfsburg iko tayari kumbakisha Micky van de Ven ikiwa Tottenham Hotspur haitakidhi bei yao ya pauni milioni 40 kumnunua mlinzi huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 22. **(Wolfsburger Allgemeine, via Express)**

### BARNES AITAKA NEWCASTLE

WINGA wa Leicester City, Harvey Barnes mwenye umri wa miaka 25, anataka kuhamia Newcastle United msimu huu wa majira ya joto. **(Football Insider)**

### FRED ABADILISHA WAKALA

KIUNGO wa kati wa Manchester United na Brazil, Fred mwenye umri wa miaka 30, amebadilisha wakala wake huku Klabu za Fulham na ya Saudi Arabia zikiwa na nia ya kutaka kumsajili **(Fabrizio Romano)**

### OSIMHEN ATAKIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inaweza kumsajili mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 24, kama mbadala wa mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 24. **(Gazzetta dello Sport, via Football Italia)**

### PULISIC AKOSOLEWA

GWIJI wa zamani wa Marekani, Landon Donovan amemkosoa winga wa Chelsea, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 24, kwa kuchagua kujiunga na AC Milan badala ya kuhamia Ligi ya Marekani, MLS. **(Fox Sports)**

### MOURINHO AMTAKA MCTOMINAY

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho anatamani kumsajili kiungo wa kati wa Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 26, kutoka klabu yake ya zamani ya Manchester United. **(Football transfers)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BAYERN YAWEKA DAU LA PILI KUMNG'OA KANE

Spurs wanabaki kuimarika na hawana nia ya kumruhusu mfungaji huyo, lakini...

**MUNICH, Ujerumani**

BAYERN Munich imetuma ofa ya pili yenye thamani ya euro milioni 80 kwa mshambuliaji, Harry Kane, ingawa Tottenham Hotspur bado imesisitiza kuwa haina nia ya kufanya mazungumzo.

Nahodha huyo wa England amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake wa sasa.

Spurs wamekuwa na uhakika wa kumbakisha Kane kwa muda mrefu ujao na tayari wamekataa ofa ya kwanza ya euro milioni 70 kutoka kwa mabingwa hao wa Ujerumani Bayern mapema msimu huu wa majira ya joto.

Tottenham hawana mpango wa kumuuza mchezaji huyo na 90minutes inaelewa kuwa hakuna bei inayoweza kuamuliwa na uongozi wa klabu huku Bayern na kocha Thomas Tuchel wakishinikiza makubaliano.

Kocha wa zamani wa Chelsea, Tuchel anataka Kane aongoze safu hiyo ya ushambuliaji na ana matumaini ya kupata dili katika miezi ijayo.

Hata hivyo, Spurs wanabakia kuimarika na hawana nia ya kumruhusu mfungaji huyo bora wa pili katika historia ya Ligi Kuu England kuondoka.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, alikuwa katika kiwango kizuri tena 2022/23, akifunga mabao 30 huku timu yake ikimaliza nafasi ya nane.

Klabu kubwa za Ulaya zimeonesha nia ya kumtaka mchezaji huyo zikiwamo Manchester United, Paris Saint-Germain na Real Madrid.

Kocha mpya Ange Postecoglou atatumaini Kane bado ataendelea katika klabu hiyo msimu wa 2023/24 utakapoanza.

Spurs wamemwongeza Dejan Kulusevki kwenye safu yao ya ushambuliaji huku pia Guglielmo Vicario na James Maddison wakitua hapo.

# PSG YAMTWAA HERNANDEZ KWA MIAKA 5




**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain imemsajili beki Lucas Hernandez kutoka Bayern Munich kwa mkataba wa miaka mitano, mabingwa hao wa Ligue 1 wametangaza.

Ada ya uhamisho haijaweka wazi, lakini vyombo vya habari vya Ufaransa viliripoti kuwa PSG walikuwa wameilipa Bayern ada ya euro milioni 40 pamoja na nyongeza kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27.

"Nimefurahi sana! Nimekuwa nikisubiri kujiunga na PSG kwa muda mrefu na hatimaye imetokea. Ni siku maalum sana kwangu na nina furaha sana kuwa hapa," alisema Hernandez katika taarifa yake.

Atletico Madrid, klabu ya utotoni ya Hernandez, pia itapokea gawio la ada kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari vya Hispania.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa alicheza mechi 107 kwa mabingwa hao wa Ujerumani tangu kuwasili kwake mwaka 2019, lakini alicheza mechi saba pekee za ligi msimu uliopita baada ya kupata jeraha la mguu kwenye Kombe la Dunia ambalo lilimfanya kuwa nje kwa muda uliosalia wa msimu.

Hernandez, mchezaji mpya wa tano kusajiliwa PSG, anaungana na viungo Manuel Ugarte na Lee Kang-in, beki wa kati Milan Skriniar na fowadi Marco Asensio.

Klabu hiyo pia ilimtimua kocha Christophe Galtier na nafasi yake kuchukuliwa na kocha wa zamani wa Barcelona na Hispania, Luis Enrique.

# Silva ataka Chelsea imsajili Dybala

**LONDON, England**

THIAGO Silva amekiri kuwa alimwomba Paulo Dybala ajiunge na Chelsea baada ya ripoti kuhusishwa na mshambuliaji huyo kuhamia Stamford Bridge.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Argentina, hivi karibuni amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Chelsea msimu huu wa majira ya joto, huku mchezaji huyo akiripotiwa kuwa na kipengele cha kuachiwa cha euro milioni 12 katika mkataba wake na klabu yake ya sasa ya AS Roma.

Akizungumza na Sky Sport Italia kuhusu tetesi hizo, nahodha wa Chelsea Thiago Silva alikiri kwamba alimuuliza Dybala kama anaweza kujiunga na The Blues hao, akisema: "Nilimwona Paulo Dybala hapa, (vyombo vya habari) vinazungumza juu yake kuja Chelsea. Nimezungumza naye na kumuuliza kama atakuja.



"Ni mchezaji wa kiwango cha kimataifa. Ningependa kucheza naye na utakuwa usajili mkubwa. Hebu tuone."

Dybala alijiunga na Roma msimu uliopita baada ya kumalizika kwa mkataba wake na Juventus, lakini amekuwa akiandamwa na majeraha tangu ahamie.

Wakati wa msimu wa 2022/23, fowadi huyo alikosa michezo 18 kutokana na majeruhi, lakini aliweza kufunga mabao 18 na kutoa pasi saba za mabao katika mashindano yote kwa kikosi cha Jose Mourinho - ikiwa ni pamoja na moja kwenye fainali ya Ligi ya Europa.

Alipoulizwa na waaandishi wa habari wa Italia katika uwanja wa ndege Jumamosi, Kocha wa Roma, Mourinho kuhusu Dybala kwenda Chelsea alijibu: "Sijui kuhusu mkataba wake."

"Lakini ni wazi nazungumza na Paulo kama ninavyofanya na wachezaji wangu wote."

Chelsea tayari imekuwa hai katika dirisha la usajili la majira ya joto, ikiwasajili washambuliaji Christopher Nkunku na Nicolas Jackson kwa jumla ya euro milioni 87.

# Greenwood kupelekwa kwa mkopo Atalanta

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imefanya mazungumzo na Atalanta kuhusu uwezekano wa kumnunua Mason Greenwood kwa mkopo, kwa mujibu wa 90min.

Greenwood alisimamishwa Man United tangu Januari 30, 2022, baada ya kushtakiwa kwa jaribio la ubakaji.


Mashtaka dhidi ya Greenwood yalitupiliwa mbali na mahakama Februari, lakini mchezaji huyo alibakia kusimamishwa na United kwa kipindi kilichosalia cha msimu uliopita, huku klabu hiyo ikifanya uchunguzi wa ndani.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ana mkataba na United hadi Juni 2025 huku klabu ikiwa na chaguo la kuongeza mkataba huo kwa mwaka mmoja.

United imekuwa ikifikiria jinsi ya kuendelea na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 na wamefanya mazungumzo na Atalanta juu ya uwezekano wa kumpeleka mchezaji huyo kwa mkopo kule Serie A.

Mazungumzo yamefanyika kuhusu uwezekano wa United kununua Hojlund huku Greenwood ikipelekwa kwa mkopo Bergamo kwa kubadilishana, ingawa inaeleweka kuwa Atletico Madrid nao wanamtaka Greenwood pamoja na Borussia Dortmund.

Greenwood amepigwa picha akifanya mazoezi peke yake wiki za hivi karibuni na hajarejea United kwa ajili ya kuanza kwa maandalizi ya msimu mpya.



# AZAM YASAKA DAWA YA KUFUTA UTEJA KWA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC ambayo imewasili salama jijini Sousse, Tunisia, kuweka kambi ya wiki tatu ya maandalizi ya msimu mpya, imesema safari hii imejipanga kuifunga Yanga kwenye mechi ya Ngao ya Jamii na kufuta uteja wa kupigwa mechi mbili mfululizo zilizopita.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat', amesema kwa sasa wapo kambini na wanafanya mazoezi ya kuweka wachezaji kwenye utimamu wa mwili, lakini watakaporejea Julai 30, mwaka huu, ndipo wataanza rasmi maandalizi ya mechi hiyo ambapo watakuwa makini mno ili wasipoteze kwa mara nyingine tena.

"Tumeiona ratiba, tunajiandaa na mechi hiyo dhidi ya Yanga, tuiheshimu ndiyo maana tunapokutana nao, wao na Simba mechi tunazichukulia uzito mkubwa, kwa sasa tupo kwenye 'pre season', tukirudi tutakuwa kama na siku nane za kujiandaa na pambano hilo.

"Ni kweli tumepoteza mechi kadhaa dhidi ya timu hiyo, lakini siyo kama wanakuwa wametuzidi sana ila wanakuwa bora zaidi yetu kwa siku hiyo, walitufunga mechi moja kwenye ligi na fainali ya Kombe la FA na siyo kama walitufunga kinyonge kila mtu aliona, mechi moja tulitoka sare. Sasa tunajipanga kwa ajili ya mechi hiyo ili na sisi tutokea na ushindi," alisema Popat.

Septemba 6, Azam ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Yanga kwenye mzunguko wa kwanza, lakini Desemba 25, mwaka jana ilipokea kipigo cha mabao 3-2, Ligi Kuu Tanzania Bara mzunguko wa pili, kabla ya kudunguliwa bao 1-0, Juni 12, mwaka huu, katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, ikiwa ni mchezo wa fainali ya Kombe la FA.

Azam itakipiga tena na Yanga Agosti 9, mwaka huu kwenye uwanja huo huo, ikiwa ni mchezo wa Ngao ya Jamii kuashiria msimu mpya wa Ligi Kuu 2023/24 kuanza.

Fainali ya taji hilo itachezwa Agosti 13, mwaka hu hapo hapo, Mkwakwani, tanga, baada ya kupata pia mshindi wa mechi ya Agosti 10, kati ya Simba na Singida Fountain Gate FC.

## Saido atoa neno msimu mpya, usajili

**Na Saada Akida**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza, amesema amerejea kivingine kwenye majukumu yake ndani ya klabu hiyo kuelekea msimu wa 2023/24.

Ntibazonkiza alimaliza msimu uliopita akiwa na mabao 17 sawa na Fiston Mayele wa Yanga, hivyo wote wakatunukiwa kiatu cha ufungaji bora msimu wa 2022/23.

Kiungo huyo mshambuliaji anaungana na wachezaji wenzake kambini kujiandaa na safari ya timu hiyo leo kuelekea Uturuki kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa 2023/24.

Akizungumza na Nipashe jana, Ntibazonkiza alisema sasa likizo imeisha na amerejea kazini kivingine kuhakikisha wanaungana na wachezaji wenzake kufikia malengo ya klabu.

Alisema anaimani msimu huu watakuwa bora zaidi ya msimu uliopita kwa sababu ya maboresho ya kikosi cha timu yao na kuamini watafanya vizuri zaidi na kufikia kile ambacho kinatarajiwa na Wanasimba.

"Likizo imekwisha na nimerejea kazini katika majukumu yetu kwenda kufikia malengo ambayo tunayahitaji ikiwamo kutwaa mataji yote ya mashindano ya ndani na kufanya vizuri zaidi kwenye michuano ya kimataifa," alisema.

Alisema anaamini viongozi wamefanya usajili kulingana na mahitaji ya timu yao, hivyo kwa kushirikiana na wachezaji wenzake wanatarajia kufanikisha malengo hayo ya msimu ujao.



Saido

## Yanga kuja na mshindo mkuu

INATOKA UK. 24

Aliongeza kuwa hayo ni mafanikio waliyopata ndani ya kipindi cha mwaka mmoja tangu amechaguliwa kuiongoza Yanga, hivyo kuwaomba mashabiki wa klabu hiyo kuendelea kumwamini kwa miaka mitatu ijayo ili kufanikiwa katika mipango yao.

"Tunaenda kuimarisha timu yetu msimu huu kwa kufanya usajili mdogo kulingana na mahitaji ya kikosi chetu, kulingana na tulipoishia kwa msimu uliopita," alisema Hersi.

Aidha, aliwataka Wanayanga kuwapa ushirikiano na kupotezea mitandao ya kijamii kuhusu mambo ambayo yanaleta mgongano baini yao na viongozi hasa katika suala la usajili wa wachezaji wa kigeni.

Kwa upande wa SportPesa, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Sabrina Msuya akimkaribisha Mwenyekiti wao wa Bodi ya Wakurugenzi, Tarimba Abbas, kwa pamoja waliipongeza Yanga kwa mafanikio hayo iliyoyapata baada ya kufungua msimu kwa kubeba Ngao ya Jamii, kisha ubingwa wa Ligi Kuu Bara, kufika fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika na kubeba FA Cup.

"Nianze kwa kuwashukuru ndugu waandishi kwa kufika, lakini kipekee niwapongeze timu ya Yanga kwa kuweza kufanya vizuri katika msimu huu wa ligi. Nafikiri kila mmoja wetu anajua kile ambacho mmefanya na kwa heshima na taadhima niwape hongera viongozi, wachezaji pamoja na benchi la ufundi," alisema Sabrina.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Tarimba alisema:"Klabu ya Yanga safari hii imepata viongozi bora na kwa mafanikio haya kila mtu anajionea maana ni mwendo wa makombe tu kila msimu, kwa misimu miwili mfululizo, ni matumaini yangu ushindi huu utakuwa endelevu.

"Ni faraja yetu sisi kama wadhamini wakuu kuona mnaitendea haki nembo ya SportPesa kwa miaka sita mfululizo. Leo tunatimiza jukumu la kimkataba kwa kuwapa bonasi ya Sh. milioni 405 kutokana na kujituma kwenu ili iwe kama motisha kwa mashindano yajayo kuelekea msimu wa mwaka 2023/24."

## Simba yataja watatu wapya

INATOKA UK. 24

mrejesho kutoka kwa viongozi wake, lakini huenda leo, Jumanne au kesho Jumatano wakatangaza mchezaji mwingine, hata hivyo jana klabu hiyo ilitangaza kumwongezea beki wa kulia, Shomari Kapombe mkataba wa miaka miwili zaidi ambapo sasa ataitumikia Simba hadi mwaka 2025.

Wakati huo huo Simba ilitarajia kuondoka leo kuelekea Uturuki kwa kambi ya wiki tatu, huku nyota wao mpya, Che Malone, akionesha kufurahishwa na mapokezi mazuri aliyoyapata, hivyo kuahidi kufanya kile kilichosababisha asajiliwe kwa kuwarudishia furaha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo.

"Kwa sasa ni mchezaji wa Simba, naahidi nitafanya kazi ya kuwapa furaha wapenzi wa klabu hii kubwa, kwani wamenipa mapokezi mazuri sana," alisema beki huyo wa kati aliyesajiliwa kutoka Cotonsport ya Cameroon.

# Michezo


Jumanne Julai 11, 2023
Nipashe




## Bayern yaweka dau la pili kumng'oa Kane

UKURASA 21

MMETISHA...




Rais wa Klabu ya Yanga, Hersi Said (kushoto), akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni 405 kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas (kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano SportPesa, Sabrina Msuya, ikiwa ni bonasi ya kufanya vizuri katika mashindano yote waliyoshiriki msimu uliopita. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA KUJA NA MSHINDO MKUU

●●●SportPesa yaijaza milioni 405/-, yawashusha presha mashabiki ikisema sasa watarajie...

**Na Saada Akida**

LICHA ya kimya kingi cha usajili mpya kuelekea msimu wa 2023/24, kutawala katika viunga vya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam yalipo makao makuu ya Yanga, uongozi wa klabu hiyo umewashusha presha mashabiki wao baada ya kusema utakiboresha kikosi hicho na kuja kivingine kikiwa imara zaidi kuliko msimu uliopita.

Hadi sasa Yanga imetangaza kukamilisha usajili wa mchezaji mmoja tu ambaye ni mzawa, beki wa kushoto Nickson Kibabage, akitokea Singida Fountain Gate FC huku watani wao wa jadi, Simba wakiwa tayari wametangaza nyota wapya watatu wa kimataifa kutoka Ivory Coast, winga Aubin Kramo Kouame, na nyota wawili raia wa Cameroon beki Che Fondoh Malone na winga Willy Essomba Onana.

Akizungumza katika hafla fupi ya kukabidhiwa bonasi na wadhamini wao wakuu, Kampuni ya Kubashiri Michezo ya SportPesa, baada ya kufanya vizuri msimu uliopita kwenye mashindano yote waliyoshiriki, rais wa Yanga, Hersi Said, alisema watakiboresha kikosi hicho kuwa bora kuliko msimu uliopita ili kuendelea kuwatendea haki wadhamini wao na kuwapa furaha mashabiki wa timu hiyo.

Alisema kwa ujumla wanawashukuru SportPesa kwa kuwa kuwakabidhi hundi hiyo ya Sh. milioni 405 ikiwa ni sehemu ya mafanikio ambayo wameyapata kwa msimu uliopita.

Hersi alisema katika mkataba wa SportPesa na Yanga ni mara mbili kutokana na kile wanachokipata kila mwezi pamoja na yale ambayo timu ikifanikiwa kutwaa ubingwa, Ngao ya Jamiii, FA Cup na mashindano ya kimataifa.

"Hii pesa kiasi cha Sh. milioni 405 ni sehemu ya kimkataba wetu wa sehemu ya pili ambayo baada ya mafanikio tuliyoyapata msimu uliopita. Hatuna shida na SportPesa kama ilivyokuwa ikivumishwa hasa Yanga tulipoingia katika hatua ya makundi hatukuweza kuvaa (jezi zenye nembo) ya SportPesa.

"Hiyo ni kutokana na sheria kutubana, hivyo hizi pesa tulizopata leo ni sehemu ya mafanikio ya mashindano ya kimataifa," alisema Hersi.

UKURASA. 23

## Simba yataja watatu wapya wakusajiliwa

**Na Adam Fungamwnago**

PAMOJA na kutangaza wachezaji watatu mpaka sasa, klabu ya Simba imesema bado haijamaliza zoezi la usajili, huku ikitangaza nafasi tatu hadi nne ambazo inatarajia kushusha 'vyuma' vipya vya kimataifa kabla ya dirisha kufungwa.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema mpaka sasa walichofanya ni kama dibaji tu, lakini bado hawajamaliza usajili kwani tangu mwanzo waliahidi kuwa wanafanya maboresho makubwa kwenye kikosi hicho na kazi ndiyo kwanza imeanza.

"Hiyo ilikuwa ni dibaji tu bado hatujamaliza usajili, kumbuka tunafanya maboresho ya kikosi chetu, kama ni gari basi tunafanya kazi ya kushusha injini tunaweka mpya, kubadilisha matairi tunaweka mapya, kupiga bodi rangi, tunabadilisha viti, tunasafisha ili kuitengeneza Simba mpya na iliyokuwa imara.

"Kuna nafasi tatu au nne hivi zimebaki, bado kiungo mkabaji tunae ila hatujamtambulisha, winga teleza ya kuingia na kufunga na pia bado golikipa na mwingine hivi, kwa hiyo wanachama na mashabiki wa Simba wakae kwa kutulia, mambo bado," alitamba Ahmed.

Akizungumzia usajili wa Che Malone, alisema wamempa mkataba wa miaka mitatu, na ndiye mchezaji ambaye aliwapa tabu sana kupata saini yake kwa sababu walikuwa wanamgombea na klabu mbalimbali za Afrika na bara la Ulaya.

"Che Malone amekuwa mnyama kwa mkataba wa miaka mitatu, kulikuwa timu nyingi zilikuwa zinamhitaji, watu wakipanda dau, zipo za Afrika na za Ulaya Mashariki, Austria, Sweden na Uswisi zilikuwa zinamtolea macho.

"Kwa mchezaji kama huyu umri wa miaka 24 anachezea Taifa la Cameroon, unajua wachezaji wa Afrika Magharibi wanaaminika sana huko kwa sababu kuna watu wameshatangulia sokoni na wamefanya vizuri, kwa hiyo alikuwa anawindwa sana, Simba tukanyang'anyana nao na kufanikiwa kumpata na siku zote mwenye kisu kikali ndiye aliyekula nyama," alisema.

Kuhusu utambulisho wa wachezaji wengine alisema bado alikuwa hajapata

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >